„Kalenga, nilijaribu kadiri ya uwezo wangu, lakini haikufaa kwa kuwa Peter na wazazi wake walikuwa na tabia mbaya sana ya kuamini kama kila kitu kinawezekana kutokana na ukwasi waliokuwa nao. Wana imani nzito sana ya kuwa kila mtu ni majehuri wa pepo ya ubwege.“

„Loh!“ Kalenga akakurupuka, „mbali ya ujeuri wao, lakini bila shaka Peter alikuwa akikupenda sana.“

„Ndiyo natambua kuwa alikuwa akinipenda, lakini si katika misingi ninayoitaka. Alikuwa akiniudhi sana kwa kufikiri kuwa angeweza kununua utu na dhamiri yangu.“ (Uk. 40)

Sie sucht Peters Vater in seinem Büro in Ministerium auf, ohne vorher einen Termin zu vereinbaren. Er empfängt sie dennoch freundlich und gibt ihr den folgenden Rat:

„Akaniambia ati: 'please kafikirie tena otherwise utajiharibia chance na privilege hii ya kuoana na Master Peter!' Halafu akaniaga bila hata ya kutaka kusikiliza zaidi mawazo yangu, nami nikaondoka,“ Josina kamweleza Kalenga ambaye alikuwa katumbua macho anamsikiliza kwa makini. (Uk. 41)

Bei der Trauung in der Kirche weigerte sie sich, das Jawort zu sprechen. Kalenga hat von sich nicht viel zu erzählen. Im Jahre 1975 wurde Mosambik von der Kolonialherrschaft Portugals frei. Kalenga wurde als Korrespondent für eine Zeitung dorthin entsandt. Er verfasste seine Berichte unter den Pseudonamen Kamarada K. Josina war eine begeisterte Leserin seiner Berichte, ohne zu wissen, wer der Verfasser ist. Heute freut sie sich zu erfahren, dass Kamarada K. in Wirklichkeit Kalenga ist. Er ist erst vor einigen Tagen aus Mosambik zurückgekehrt. Er war es, der den älteren Bruder ihres Vaters und seine Frau zu ihrem Haus gebracht hatte, als sie aus Mosambik kamen.

Josina ist zurück in ihrem Elternhaus. Nuru freut sich. Sie plaudern miteinander. Josina hat ihre Lehrstelle an der St. Joseph's Secondary School verloren. Sie ist um ihre Zukunft besorgt. Sie wartet auf Kalenga, der längst hätte kommen sollen, sie abzuholen. Heimlich hört sie ihrem Vater zu, der mit seinem älteren Bruder aus Mosambik spricht.

„Kaka, usisikilize sana maneno ya Josina. Nafikiri kaachishwa kazi kwa ujeuri wake tu!“

„Mdogo wangu, usikimbilie kuamua mambo namna hiyo. Unajuaje kama kufukuzwa kwake ni njama? Hujui kwamba hii inaweza kabisa kuwa ni kisasi cha huyo Waziri kama asemayo Josina?“

„Mimi siamini kaka, Bwana James namfahamu sana. Ni mtu mwenye heshima yake na ambaye hawezi kufanya kitu cha upuuzi kama hiki. Tabia ya Josina naifahamu sana, ni machachari sana tangu utotoni. Naamini kwamba Wacuba walizidi kuiharibu tabia yake alipokwenda kusoma huko.“

Josina hakutaka kusikiliza zaidi ubishi huo. Akatambua wazi kwamba donda ndugu lililokuwa limeikorofisha nyumba yao kwa muda mrefu na baadaye likatafutiwa dawa, lilikuwa limeanza kutoa usaha. (Uk. 44)

Einige Tage sind nach dem Gespräch im Hilton Beach Hotel vergangen. Josina sitzt in ihrem Zimmer im Elternhaus. Sie blättert die Artikel durch, die Kalenga in Maputo (früher Lourenço Marques) verfasst hat. Ein Artikel weckt ihre Aufmerksamkeit besonders, nämlich „Ukombozi wa wanawake ni harakati za kitabaka.“ (Uk. 45). Darin kommt er auf den Beitrag der Frauen zum Aufbau eines neuen Mosambik zu sprechen.

Josina und Kalenga sind seit der Jugendzeit befreundet. Damals hieß sie Lulu und er Akida. Sie änderten ihre Namen beim Eintritt in die St. Joseph's Secondary School. Aus Lulu wurde Josina und aus Akida Kalenga. Josinas Vater wurde aber wütend, gebrauchte das starke Wort „laana“ (Fluch) und sagte: „Mtoto wewe umelaaniwa sana“ (Uk. 45). Doch er gab schließlich nach und gewöhnte sich an die neuen Verhältnisse. Josinas verstorbene Mutter hatte ihn bewogen, sich mit der Tochter zu versöhnen.

„Sielewi kwa nini Baba analilia sana jina la Lulu. Mimi, Mama, nadhani uhuru wa majina aachiwe yule anayetwa maana yeye ndiye anayehusika zaidi. Mama hivi unaelewa maana ya Lulu? Ni kitu cha thamani sana, pambo la kuvutia. Mimi sioni kama jina hili litakuwa na uzito wowote siku ya usoni,“ Josina akamweleza Mama yake.

„Mwalimu ametueleza sana kwamba majina kama haya yanaendeleza hali ya kuwadhalilisha wanawake. Baadala ya kuonekana kuwa watu wanafikirikwa kuwa maua tu ya kuwapendeza wanaume. Ndiyo maana mimi na wenzangu tukaamua kujiandikisha majina mapya, mimi nikachagua jina la Josina, mwanamke mpigania Uhuru wa Msumbiji.“ (Uk. 46)

Auch Kalengas Vater gefiel die Namensänderung nicht, aber aus einem anderen Grund. Er identifizierte den Namen Akida mit Arabern und dem Islam, den Namen Kalenga abschätzig mit den „Wa-Bara“. Wabara war in Sansibar die abschätzig Bezeichnung für Schwarzafrikaner vom Festland Tanganyika, die als Wanderarbeiter auf die Insel kamen.

„Mtoto laana kabisa wewe. Umethubutuje kubadili jina uliloadhiniwa na wazazi wako? Umerukwa na akili?“ Sheikh Mabruki akafoka huku kapandwa na ufufufuru.

„Ati Kalenga! Jina gani hilo lisilo na hadhi ya Kiislamu kama si la Kikafiri! Mtoto uliyekuzwa

katika nyumba safi ya Kiislamu unaonyesha dharau kwa wazazi wako na dini namna hiyo! Sheikh Mabruki alisikika akifoka. (Uk. 46)

Kalenga hatte jedoch keine Gelegenheit, seine Absicht zu begründen. Er hatte den Namen nicht willkürlich geändert, sondern weil er sich mit dessen Bedeutung nicht identifizieren wollte.

Alikuwa kachukia sana maana sababu za kubadili jina alikuwa nazo na alizona ni za msingi. Kalenga aliliona jina la Akida kuwa kumbukumbu ya unyapara na utwana wakati wa ukoloni wa Mjerumani. Hivyo akaamua kujiita Kalenga jina maarufu la ngome ya Mtemi wa Wahehe Mkwawa aliyejitoa mhanga kupigana dhidi ya ukoloni wa Mjerumani. (Uk. 47)

Angeregt wurde der Entschluss, die Namen zu ändern, vom Geschichtslehrer Kamala. Er erläuterte die Schäden, welche die Kolonialherren in Deutsch-Ostafrika angerichtet haben. Er nannte sie: „Madhambi ya Ukoloni na athari yake katika jamii.“ (Uk. 47)

Während Josina diese Überlegungen anstellt, kommt Kalenga in einem Cortina angefahren, einem Dienstauto der Tageszeitung Kioo cha Bia. Binamu begrüßt ihn herzlich auf portugiesisch. Sie setzen sich und plaudern. Sie kommen auf Josinas Entlassung zu sprechen. Sie gibt Kalenga den Bescheid zum Lesen. Die Überschrift lautet: „Kuachishwa kazi mara moja“ (Uk. 50). Kalenga liest den Bescheid.

Akashituka kidogo alipofikia aya ya mwisho iliyokuwa imeandikwa, „Kutokana na utovu wa heshima kwa wakuu wako wa kazi, msimamo wako kisiasa uliopotoka, taswira ya mapinduzi yenye kilema nayo uliyo na utukutu wako wa kutaka kuhujumu na kuchafua imani ya wanafunzi kisiasa, Bodi ya Wadhamini ya Chuo cha Forodhani, inaamua kukuachisha kazi mara moja bila ya kupata marupurupu ya aina yoyote ile.“

Kalenga akaendelea kusoma huku wote wakimsikiliza kwa makini, „Tunakutakia kila la kheri katika maisha yako mpya ingawa papo hapo tunakuasa kuwa usipobadili mwenendo wako, utajiletea madhara na madhila yasiyoweza kuelezeka kwa urahisi.“

Mwishoni mwa barua hiyo kulikuwa na sahihi ya Mwenyekiti wa Bodi, Boaz Kasongo ambaye pia alikuwa Mkurugenzi wa *Disco Fever Haven*, jumba la starehe na muziki mjini Dar.

Kalenga akavutiwa na orodha ya majina ya wakurugenzi wa Bodi hiyo waliokuwa wamepelekwa nakala za barua hiyo. Akaliona jina la Waziri Knox James, *Sir Henry Mwapaker* na Mhariri wa gazeti la *Kioo cha Bia*, Bubu Ogala.

„Pole sana Josina,“ Kalenga akazianika hisia zake na kumrejeshea Josina barua yake.

„Vipi unaionaje barua hiyo? Si ni ujeuri tu wa huyu dada yako? Kapata kazi, kaanza kulewa madharaka, kawanyea wakuu wake wa kazi waliompeleka Ulaya kusoma na sasa kaumwaga unga!“ Simango akaanza kutapika maneno.

Kalenga alitaka kusema neno lakini akasita, Mzee Binamu huku akiwa kanuna, akamgeukia Mdogo wake na kumwangukia kwa hasira.

„Simango, mtoto kafukuzwa kazi, unazidi kumwongeza uchungu kwa maneno yako yasiyo na

msingi. Hivi, ulimwona Josina akiwanyea wakuu wake wa kazi? Ulisikia wapi kuwa alikuwa kalewa madharaka? Si vizuri hivyo Simango!“

„Kaka nakuomba usinitukane mbele ya watoto. Wewe unafikiri watu wanafukuzwa kazi kiholela tu hapa nchini? Lazima kuna sababu. Mbona mwenziwe hapa badala ya kufukuzwa kapandishwa cheo? Ni mpuuzi tu mtoto huyu, lazima niseme kwa pumzi ya mzazi! Kwanza ... “

„Wazee wangu,“ Kalenga akamkata kalima Simango, „Miye nadhani ni mapema mno kuweza kulitalii suala hili kwa mapana na marefu na kuipata dhati yake. Si kwamba namtetea Josina, la hasha, isipokuwa naona uwezekano mkubwa wa uonevu.“

„Uonevu utoke wapi!“ Simango akarukia. Kalenga akasita kidogo halafu akaendelea, „Majina niliyoyaona kwenye barua hiyo ya wajumbe wa Bodi yananipa wasiwasi. Utakuta kuna watu au mtu mwenye kinyongo fulani na Josina. (Uk. 50-52)

Kalenga wird zum Essen eingeladen. Er lehnt jedoch höflich ab, denn er muss zur Arbeit. Dort wartet Chefredakteur Buba Ogola auf ihn. Er gibt ihm eine Kopie des Briefes, den Kalenga im Hause Josinas schon gelesen hatte. Kalenga überfliegt ihn und gibt ihn Buba Ogola zurück.

„Umesoma na kuiielewa?“ Ogola akauliza kwa mshangao kidogo.

„Tena sana,“ Kalenga akajibu.

„Je, unaionaje?“

„Naiona ya kawaida sana.“

„Una maana gani?“

„Nina maana ya kuwa barua hii inazungumzia mambo ya kawaida sana, mambo ya kila siku. Mtu kufukuzwa kazi, kwangu si suala la ajabu sana au habari ya kulisimua,“ Kalenga akajibu.

Mhariri Mkuu akashituka kidogo. Akaangalia darini kwa muda kama mtu mwenye mawazo mazito. Kalenga akaamua kuzikatisha ndoto za mchana za Ogola.

„Vipi Mhariri Mkuu, ulitaka habari hizi tuzichapishe gazetini?“

Ogola akaitikia kwa kichwa halafu akaongeza, „Barua yenyewe imekuja na agizo kutoka Waziri Msaidizi wa Utabiri na Visima ambaye pia ni Katibu wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo hicho kuwa lazima ichapishwe.“

Kalenga akanwangalia Mhariri Mkuu wake kwa muda kidogo halafu akanena, „Kwanza naomba unifahamishe, hivi na wewe umo katika Bodi hiyo maana nimeliona jina lako.“

Ogola akaitikia tena kwa kichwa. Dakika mbili hivi zikapita bila mtu kusema neno.

„Miye nadhani,“ Kalenga akaanza, „umuhimu wa kuchapisha habari hii haupo maana ni watu wengi sana wanaofukuzwa kazi karibu kila siku na hatuandiki habari zao, tena wenye madaraka makubwa kumpita huyu mwalimu. Pengine itakuwa vizuri wewe, ukiwa mjumbe wa bodi hii, ufafanue zaidi uzito wa kufukuzwa kwa mwalimu huyu wa umma.“ (Uk. 53-54)

Kalenga gibt Chefredakteur Ogola den Rat, keine Anweisungen von Politikern anzunehmen, sondern sich auf die Ergebnisse eigener Ermittlungen zu verlassen. Er lehnt die Veröffentlichung des Briefes im Kioo cha Bia ab.

Kalenga hat einen Termin mit Josina im Hotel Amana. Er ist deprimiert, betrübt. Beim Autofahren hielt ihn ein Polizist auf, warf ihm vor, dass er betrunken fährt und nahm ihm den Führerschein ab. Während er zwei Tage in Haft saß, wurde der Bericht über Josinas Entlassung

im Kio cha Bia veröffentlicht. Josina ist wütend. Sie verabschiedet sich. Kalenga ist allein. Er trinkt noch ein Bier. Ein Gast kommt herein. Alle Angestellten stehen auf und begrüßen den Neuen. Es ist Peter, der Sohn des Ministers James Knox. Peter setzt sich zu Kalenga. Sie kommen ins Gespräch. Sie plaudern über ihre Jugendjahre in der St. Joseph's Secondary School, über Kalengas Arbeit in Maputo sowie die Reizthemen Kommunismus und China. Kalenga bekennt sich zu Ujamaa und lehnt jede Art von Kommunismus ab. Ein weiteres Reizthema ist die Quelle und Verteilung von Wohlstand. Kalenga versucht herauszufinden, woher Peter das Geld für sein Auto bekommen hat.

„Kwa mfano wewe umepata wapi gari hilo jipya?“

„Nimenunua,“ Peter akajibu.

„Ulipata wapi fedha za kununulia gari la gharama kama hilo?“

„Alaa, hivi unaona ajabu. Baba yangu alinipa, ana mshahara mkubwa na tunafanya *business* ndogondogo.“

Kalenga akacheka na kuendelea, „*Business* ndogondogo! Si Mzee wako ni Waziri? Kwa vile yeye kiongozi ingempasa kuonyesha mfano mzuri kwa watu kuwa hana njia nyingine za pembeni pembeni za kujipatia mali za ziada. Nina hakika anaajiri watu katika hizo *business* ndogondogo na anawalipa ujira. Hivyo yeye anaajiri, anamiliki njia za kuzalishia mali hivyo hafuati miiko ya uongozi kufuatana na siasa yetu. Umeuelewa ubepari uchwara sasa na jinsi unavyorudisha nyuma juhudi za kuijenga jamii yetu?“ Kalenga akauliza.

Peter akasimama kwa hasira bila kujibu. Akamwangukia Kalenga kwa muda, mara gari moja aina ya *Benz* likasinzilia mwendo pole pole hadi lilipofika kwenye mlango wa hoteli hiyo likasimama. Akatoka Mzungu mmoja mwenye upara mkubwa uliokuwa ukimeremeta kwa taa kali za hotelini hapo. Peter akamwangukia Mzungu huyo, halafu akamgeukia Kalenga.

„Mgeni wangu kafika, lakini Kalenga unajipalia makaa bure maana unatukana watu. Mimi ni rafikiyo, tumesoma wote, lakini mtu mwingine hawezi kuvumulia. Kalenga umepotoshwa sana na utabakia hivyo hivyo nyuma ukiendelea kuabudu nadharia zisizo na msingi“, Peter akabubujika maneno, akaondoka kumfuata mgeni wake. (Uk. 62)

Kalenga beobachtet Peter aufmerksam. Peter begrüßt seinen Gast, einen Europäer. Kalenga glaubt das Gesicht des Europäers zu kennen und seufzt leise und traurig: „Wanaiuza nchi hiyo.“ (Uk. 62)

Chefredakteur Bubu Ogala betritt Kalengas Büro. Er bittet ihn in sein eigenes Büro. Sie diskutieren über die Informationsflut zu dieser Zeit der Wahlen und die grosse Arbeitsbelastung. Plötzlich wechselt Ogola das Thema und kommt auf eine heikle Frage zu sprechen.

„Ah, pole sana Kalenga, nasikia ulitiwa ndani. Mimi kwanza nilidhani ulikuwa uko nyumbani unaumwa. Hivi ulikosa nini?“

Kalenga akakunja uso kidogo na kumjibu Ogola kwa swali vilevile, „Na mimi nilidhani ulikuwa na habari. Nani aliyekueleza kuwa nilitiwa mbaroni Ndugu Ogola?“

„Nsa ndiye aliyenifahamisha juzi jioni. Nikaenda moja kwa moja kituo cha Polisi kujaribu kukutoa, lakini walikataa katakata.“

Nsa alikuwa mpiga picha mkuu wa gazeti la *Kioo cha Bia* ambaye Kalenga alimpigia simu mara tu alipofikishwa kituo cha Polisi. Walikuwa marafiki wa siku nyingi waliokuwa wakiheshimiana sana.

Maneno ya Ogola yakaonyesha wazi kuyumbayumba kwa uongo. Kalenga akawasha sigara na kuanza kuvuta bila kusema neno zaidi.

„Jana kwa bahati mbaya,“ Ogola akaendelea, „nikalazimika kufuatana na ujumbe wa serikali ya Marekani kwenda mbuga za wanyama huko Manyara, la sivyo ningelipigana hadi utoke. Vipi, ulikosa nini maana Polisi wakakataa kunieleza.“

„Kwa kweli hata mimi sielewi mpaka dakika hii,“ Kalenga akajibu kwa mkato.

„Loh, pole sana Bwana. Huu ni uonevu ambao hatuwezi kuuvumilia. Nitajaribu kuongea na Waziri wa Polisi ili upuuzi huu usiendelee.“

Kalenga hakusema neno. Alishaongea na Nsa ambaye alimweleza kuwa Ogola hakujishughulisha hata kidogo baada ya kuelezwa juu ya mkasa huo. Kalenga akatambua wazi kuwa Ogola alikuwamo katika kupanga njama hiyo.

„Unaonaje kama nikizichapisha habari hizi za kuonewa kwangu gazetini?“ Kalenga akamchokoza mhariri wake.

Ogola akashituka kidogo halafu akamsihi Kalenga asichukue hatua hiyo.

„Sioni kwa nini tuchapishe habari hizo. Nadhani litakuwa jambo la busara kumwona Waziri wa Polisi, nina hakika atachukua hatua kali zifaazo,“ Ogola akasema huku akikwepesha macho yake yasikutane na ya Kalenga.

Kalenga akataka kufunua mdomo ili kujibu lakini Ogola akamkatisha kwa kubadili mazungumzo.

„Halafu Kalenga, Waziri Msaidizi wa Utabiri na Visima alipiga simu hapa kwangu leo asubuhi kutaka kuongea nawe, lakini hukuwepo. Sielewi anakutakia nini, lakini alisema angependa mwonane.“

Habari hii zikamshitua kidogo Kalenga. Alikuwa hafahamiani kabisa na Waziri huyo na wala hakuwa na uhusiano wowote naye. (Uk. 63-64)

Kalenga kehrt in sein Büro zurück, durchblättert die vielen Nachrichten, verabschiedet sich von seinen Kollegen und begibt sich ins Büro von Mzee James Knox im Ministerium von Wizara ya Utabiri na Visima. Es ist ihm zuwider, aber er muss es tun. Die Sekretärin begrüßt ihn zwar höflich, nimmt ihn aber sonst kaum zur Kenntnis. Sie ist stark geschminkt, trägt ein schönes vornehmes Kleid und spricht Kiswahili vermischt mit amerikanischen Englisch. Als Kalenga sich vorstellt, wird sie sofort aufmerksam. Mzee James Knox kommt heraus, verabschiedet sich von seinen Gästen, die graue Anzüge tragen, und heißt Kalenga in sein Büro willkommen. Das Büro ist prunkvoll eingerichtet. Er beginnt gleich mit einer Frage.

„Wewe ndiye unayejiita Kamarada Kalenga Mabruki?“

„Sijiiti hivyo isipokuwa naitwa kwa jina hilo,“ Kalenga akajibu kwa ujeuri kidogo.

„Vyema sana, nimesikia sana habari zako hivyo nikapenda kukuona. Hivi wewe kabila gani?“

Swali hilo lilimshangaa sana Kalenga. Hakuwa anatazamia swali finyu la aina hiyo kutoka mdomoni kwa kiongozi ambaye ana jukumu la kudumisha umoja wa watu.

„Mimi ni Mswahili,“ Kalenga akajibu.

„Kila mtu hapa ni Mswahili kijana, hata mimi. Ninachotaka kujua ni kabila lako.“

„Nasikitika Bwana Waziri kuwa nitashindwa kukujibu maana sina imani kabisa na suala lolote linalohusiana na ukabila.“

Jibu la Kalenga lilimudhi sana Waziri. Mashavu yake yaliokuwa yamenona mithili ya nundu ya ng'ombe yakaanza kutetemea kwa hasira. Akamtupia Kalenga jicho la ghadabu kali hadi Kalenga akaanza kutokwa na jasho jembamba polepole.

„Ama kweli wewe kijana jeuri sana. Hata hivyo si kitu. Nimekuita hapa kukuasa. Nataka unielewe kwamba sitakuita tena kama nilivyofanya leo. Nataka ubadili mara moja mwenendo wako wa uchochezi na kupinga mapinduzi yetu ya kijamaa, la sivyo utajiharibia maisha yako na kazi yako vilevile,“ Waziri James akafoka huku akitweta kwa hasira.

„Kwa wadhifa niliopewa na Chama wa Ukatibu wa Konseli ya Nidhamu ya Wanafanyakazi

Nchini, nimepata malalamiko mengi sana kuhusu mwenendo wako uliooza kwa kipindi kifupi ulichokaa hapa.“

Kalenga akashutuka kidogo kusikia kwamba Waziri James pia alikuwa Katibu wa Konseli ya Nidhamu.

„Hivi watu wengine wa kushika vyeo hivi hakuna? Mtu mmoja huyo awe Waziri, Katibu wa Bodi ya Wadhamini ya Chuo cha Forodhani, Katibu wa Konseli, Mjumbe wa Kamati ya Uvuvi wa Kitaalamu na kadha wa kadhaa. Mtu mwenyewe ana vijibishara vya binafsi chungu nzima, hivi kweli ana muda wa kulitumikia taifa kwa dhati?“ Kalenga akajiuliza kimoyomoyo

„Hili ni onyo la mwisho. Umenielewa?“ Waziri James akamuuliza Kalenga.

„Sijakuelewa ila umenishangaza sana,“ Kalenga akajibu huku akionyesha wingi wa mawazo.

„Kama umeshangazwa, endelea kushangazwa utajikuta unashangaa zaidi. Haya (u)niondoke ofisini kwangu,“ Waziri akapasuka.

Kalenga akanyanyuka polepole na kuondoka huku akili yake imevurugika mchafu koge. (Uk. 65-66)

Kalenga schaut auf die Uhr. Es ist ungefähr elf Uhr vormittags. Er beeilt sich zu seinem Parkplatz. Er kommt dort an. Er ist fassungslos. Das Dienstauto ist nicht mehr da. Er sucht es überall in der Umgebung, findet es aber nicht. Er kommt zurück. Er sieht einen älteren Mann dort stehen, wo er sein Auto geparkt hatte. Kalenga redet ihn an. Der Mann schweigt, dreht sich um und geht in das Gebäude des Ministeriums, wo Kalenga gerade einen Termin mit Minister James Knox hatte. „Wurde dieses Auto gestohlen, oder war es eine List?“ fragt sich Kalenga. Er beschließt den Fall der Polizei zu melden. Er hört die sanfte Stimme eines Jungen, der geröstete Erdnüsse verkauft. Der Junge trägt schmutzige zerrissene Kleider und ist schlecht ernährt.

„Kijana, jina lako nani?“ Kalenga akajikuta anamuuliza kijana huyo.

„Naitwa Kitwana Sefu,“ Kijana huyo akajibu.

„Hebu niambie kweli Kitwana, wazazi wako wanafanya kazi gani?“

„Kaka, mimi sina (wala) wazazi wala ndugu, nd'o maana nashindwa kukujibu,“ Kijana huyo akasema kwa kwikwi kidogo. (Uk. 66-67)

Der Junge erzählt Kalenga seine Lebensgeschichte. Er war ein Findling. Ein allein lebender Mann hatte ihn aus einem Krankenhaus im Stadtteil Mnazi Mmoja in Dar-es-Salaam zu sich genommen und großgezogen. Doch dieser Ziehvater wurde eines Tages von einem Auto überfahren, kam ums Leben und Kitwana blieb allein zurück.

„Sasa Kitwana, hii biashara ya karanga inakusaidia kweli kupata fedha za kutosha kwa kula na kuvaa?“

„Hapana Mzee,“ Kitwana akajibu huku anaangalia chini.

„Karanga zenyewe si zangu, namuuzia tu mtu ambaye hunilipa mshahara kila siku.“

„Ni nani huyo na anakulipa kiasi gani kwa siku?“

„Sijui kama utamfahamu, ni mwanamke mmoja mke wa Mzee Mwapaker. Yeye ananilipa kila siku shilingi mbili.“

Kalenga akapigwa na butaa asiweze kuamini masikio yake. „Hapana siwezi kuamini, mke wa Mwapaker, Meneja Mkuu wa Kiwanda cha Sufuria za Chai anaweza kuwa mnyama kiasi hiki kwa uroho wa fedha tu?“ Kalenga akajiuliza kwa hasira.

„Hivi unasema ni kweli Kitwana?“ Kalenga akauliza.

„Ndiyo, ni kweli. Ametuajiri vijana wengi kidogo. Yeye hupita kila asubuhi na gari kutugawia karanga ambazo tunaziua. Jioni tunampelekea fedha na karanga zinazobaki, halafu anatulipa.“

(Uk. 67)

Kalenga gibt Kitwana etwas Taschengeld für das Mittagessen, verabredet mit ihm einen Termin im Redaktionsbüro von Kioo cha Bia, und macht sich auf den Weg. Doch ihm fällt etwas ein und er kehrt zu Kitwana zurück.

Kabla hajapiga hatua nyingi, wazo jipya likamjia kichwani, akageuka na kumwita Kitwana.

„Kitwana, ulikuwapo sehemu hii tangu asubuhi?“

Kitwana akaitikia kwa kichwa. Kalenga akamuuliza kama aliliona gari moja dogo la rangi nyeusi upenuni mwa jengo la Wizara.

„Una maana gari nililokuona unaendesha ulipofika hapa?“ Kitwana akauliza.

„Ewaa.“ Moyo wa Kalenga ukatuta kwa kasi. „Je, hukumwona mtu mwingine akilichukua?“

Kitwana akainamisha kichwa kidogo akajaribu kukumbuka. „Ndiyo, namkumbuka. Ulipoingia tu ofisini humo, watu watatu wakatoka na kuondoka na gari hilo. Mimi nilifikiri uliwaazima.“

„Unaweza kukumbuka nguo walizokuwa wamevaa?“ Kalenga akaongeza udadisi.

„Ndiyo, walikuwa wamevaa suti za kijivu. Nawakumbuka sana kwa sababu walinunua karanga kwangu,“ Kitwana akasema.

„Ahsante sana Kitwana, lakini usisahau kuniona kama nilivyokueleza,“ Kalenga akasema na kuondoka kwa haraka. (Uk. 68).

Kalenga meldet den Autodiebstahl bei der Polizei. Dort wird er gefragt, ob er jemanden in Verdacht habe.

„Sasa Ndugu, kuna mtu yeyote unayemshuku kuwa ndiye aliyelipora gari hilo?“ askari akauliza

„Ndiye yupo, ni Knox James, Waziri Msaidizi wa Utabiri na Visima,“ Kalenga akasema.

Jibu hilo, likamfanya askari aliyekuwa akiandika taarifa hiyo adondoshe kalamu yake kwa hofu, askari wengine wawili waliokuwa karibu wakishughulikia kazi zingine, wakaachana kwa mshangao.

„Una hakika na jibu lako Ndugu?“ askari mwingine mfupi aliyekuwa na kipara kikubwa akauliza.

„Ndiyo nina hakika kabisa. Ninayemshuku ni Knox James,“ Kalenga akasisitiza.

„Loh, Ndugu naona kesi yako ni ngumu sana kwetu sisi. Sisi ni watu wadogo sana, tunaogopa kushughulikia kesi zinazowahusu watu wazito kama hao la sivyo tutamwaga unga. Ngoja tumwite Afande, pengine atakushughulikia,“ askari huyo akasema na kuingia kwenye ofisi iliyokuwa na kibao kilichoandikwa, „KAMANDA WA KITUO.“

Mara askari mmoja mnene mwenye kitambi kilichotutumka kama puto alitoka ofisini huku anapumua kwa nguvu akamsogelea Kalenga.

„Jina lako nani kijana?“

„Naitwa Kalenga Mabruki.“

Kusikia jina hilo, Kamanda yule alikunja uso wake kidogo, akamkazia macho Kalenga.

„Siye wewe tuliyekutia ndani hivi majuzi kwa kuendesha gari hali umelewa?“

„Ndiyo na hapana,“ Kalenga akajibu.

„Una maana gani kijana?“

„Nina maana ya kuwa sikutiwa ndani kwa sababu ya ulevi, bali kwa sababu nyingine mnazozijua.“

„Ok,“ Kamanda huyo akasema, „tuache mambo ya zamani, tugange na yaliyopo. Ehe, unasema una shida gani?“

Kalenga akarudia tena kumweleza jinsi gari la ofisi lilivyotoweka baada ya kukaa dakika chache

tu ofisini kwa Waziri James.

„Kwa vile ulikuwa ofisini kwa Waziri nd'o unamshuku wizi?“ Kamanda akamuuliza Kalenga.

„Si kwa sababu hiyo, ila ni kwamba Waziri nilimkuta na watu watatu ambao baadaye walitoweka na gari hilo, si ajabu kwa amri ya Waziri,“ Kalenga akaeleza.

„Sikiliza kijana, usijipalie makaa bila sababu. Una hakika kuwa gari hilo limeibiwa na watu hao? Vilevile una hakika juu ya uhusiano wa watu hao na Waziri?“ (Uk. 69)

Kalenga beharrt auf seinem Verdacht. Der Polizeibeamte wird wütend und geht in sein Büro zurück. Kalenga wird hinausgewiesen. Plötzlich stehen alle drei Polizisten stramm und salutieren einem jungen Offizier, der gerade eintritt. Es ist der Kamanda Mkuu Msaidizi (Stellvertretende Polizeidirektor). Er verlangt nach dem Beamten, der gerade mit Kalenga gesprochen hat. Er fordert von ihm, dass der Fall innerhalb von drei Stunden dem Gericht vorgelegt werde. Der Kamanda Mkuu Msaidizi kommt Kalenga bekannt vor.

Kamanda Mkuu Msaidizi huyo akaisogelea meza ya maulizo na kuanza kusoma ripoti ya Kalenga juu ya wizi wa gari. Akashituka kidogo na kuacha mdomo wazi baada ya kuisoma ripoti hiyo kwa muda, halafu akamgeukia Kalenga.

„Hivi wewe ni Kalenga? Kalenga Mabruki? Kamanda huyo akapiga ukelele wa furaha na kumkumbatia Kalenga kwa nguvu.

Akili ya Kalenga ikaruka huku na huko kwa haraka kujaribu kukumbuka sura ya Kamanda huyo aliyekuwa kakumbatia, hatimaye akafanikiwa. Alikuwa Hamisi Mkela, rafiki yake mkubwa tangu utotoni ambaye alikwenda Urusi kusomea ufundi wa ndege na urubani kwa miaka mingi.

„Hamisi, unajua ulinitoka kabisa?“ Kalenga akasema huku akitweta kwa furaha.

„Hata mimi Kalenga, nimestushwa tu na ripoti hii kuhusu janga lililokupata,“ Kamanda Hamisi akaeleza huku bado kamshika Kalenga mabegani.“ (Uk. 71)

Kalenga und Kamanda Mkuu Hamisi Mkela waren beide in der St. Joseph's Secondary School, aber jetzt ist nicht die passende Zeit, darüber zu sprechen. Er verspricht Kalenga den Fall in die Hand zu nehmen. Beide steigen in ein Dienstauto der Type Peugeot 604 ein. Sie fahren zur Dienststelle, bleiben kurz dort und fahren danach zu Mkelas Wohnung. Sie plaudern eine kurze Weile, danach kehrt jeder sein Büro zurück.

Josina sitzt nachdenklich in ihrem Elternhaus. Sie ist müde. Nuru ist unterwegs, Gemüse und Gewürze für das Mittagessen zu kaufen. Josina geht ins Zimmer ihrer Tante Selina, die gerade eine Matte flicht. Sie kommen ins Gespräch. Es kreist um Kalenga und Minister James Knox. Heute ist der Fall vor Gericht gebracht worden. Unbeabsichtigt schweift Josinas Blick zum Bild ihrer Mutter an der Wand. Josina war im Bezirk Kisutu im Gerichtssaal. Dort versteckte sie sich unter den Beobachtern, damit der Minister, seine Frau und ihr Sohn Peter sie nicht sehen. Das Gesicht des Ministers war von Zorn und Scham geprägt. Er stand schwach und hilfsbedürftig auf, ging zum Pult und antwortete die Fragen, die ihm gestellt wurden. Er wurde ohne Kautionsfreigelassen und fuhr mit seinem Auto der Type Audi Fox nach Hause.

Josina ist sich der Gefahr bewusst. Minister James Knox wird diese Schande nicht einfach hinnehmen. Er wird sich rächen. Kalenga wird dies zu spüren bekommen. Josina denkt über diese Ereignisse in der Stille ihrer Wohnung nach. Mzee Binamu ruft sie. Er begleitet sie in die Wohnstube, wo ihr Vater und Onkel Komba schon auf sie warten.

Kimya kirefu kikafuatia. Simango akamwangalia kaka yake, halafu akamgeukia binti yake Josina.

„Binti yangu, sasa naamini kuwa James si mtu mzima wa kumthamini. Nilidhani ni mtu mzima ambaye angelichukulia mambo yote kiutu uzima, kumbe sivyo. James ni mtoto, kifaranga hasa. Vipi mtu mzima na akili zake atake kuzoa maji yaliyomwagika mchangani?“

Binamu akatabasamu halafu akainua macho kumwangalia Simango, „Nashukuru kuwa mdogo wangu umeelewa sasa. Mpanda ngazi na msuka ngazi, kamwe hawashikani mikono!“

„Mwanangu,“ Simango akamgeukia Josina, „sasa hivi tulikuwa tunaongea na Baba zako hapa kuhusu janga lingine. Tumenyang'anywa leseni yetu ya biashara. Kijiduka chetu sasa wamekiua!“

Josina akashituka. Akamkodelea macho Baba yake huku hayaamini masikio yake.

„Bahati nzuri aliyekuja kuchukua leseni yenyewe ni rafiki yangu Mapungu, Katibu Kata, ambaye kanijulisha ni James aliyeniangusha Baba yako!“

„Kaka,“ Simango akamgeukia Binamu, „nimeshangazwa sana na kitendo cha James. Sijui anataka nini kwangu. Kama ni mahari aliyotoa kwa harusi ambayo haikufanyika, nilishamrudishia. Sasa sijui anataka nini!“

Kwa hasira, Simango akasimama na kutokomea chumbani kwake. Josina vilevile, alitaka kuondoka, lakini Binamu akamshika mkono.

„Unataka kwenda wapi?“

„Nataka kupunga upepo kidogo nje,“ Josina akajibu.

Kabla Josina hajatoka sebuleni, Nuru akaingia huku amechukua mfuko wa pilipili na binzari.

„Dada, unakwenda wapi tena na hali chakula kitakuwa tayari hivi punde?“ Nuru akamuuliza dada yake.

„Nitakuja Nuru, napunga upepo mara moja,“ Josina akasema na kuondoka.

Safari ya Josina haikuwa na ramani hata kidogo, alikuwa anataka tu kutembeatembea mitaani alimradi kupunguza uzito wa mawazo aliyokuwa nayo kichwani.

„Njama zilianza kwangu mimi, zikamkimbilia Kalenga na sasa zimemwangukia Baba. Sijui tutafika wapi!“ Josina akawaza. (Uk. 77-78)

Josina sitzt am Strand auf einem Stein und denkt nach. Sie denkt an ihre Schulzeit und an ihre Jugendfreunde in St. Joseph. Einer von ihnen war Liston. Eines Tages lud Liston sie zu sich, gab ihr ein Getränk mit einem Betäubungsmittel und entjungferte sie. Auch seine Freunde, die er eingeladen hatte, waren daran beteiligt. Am folgenden Morgen tat Liston, als ob er von diesem Betäubungsmittel nichts wisse.

Peter kommt bei seinem gewohnten Spaziergang vorbei. Er sieht Josina und bittet sie um ein Gespräch.

„Josina, nimekuwa naomba kila siku nikutane nawe ili tuweze kuongea. Kwanza kabisa, naomba tusahau ya kale, tugange na yaliyopo na yajayo. Josina, miye nasikitika sana kwa taabu unazozipata, maana miye bado nakupenda, licha ya yote yaliyotokea.“

„Uongo wa nini Peter! Unanisikitikiaje na hali wewe nd'o usukani wa matatizo yangu? Nakuomba usijaribu kunisikitikia kwa vile nimezoea sasa kuyamudu na kuyabeba matatizo yote hayo peke yangu.“

„Sivyo hivyo Josina, yote hayo yanatokana na hasira za wazazi, si mimi hata kidogo. Josina, miye bado nakupenda. Waswahili hunena, pendo ni kama mkondo wa maji, ni vigumu kuuzuia.“

„He, Peter na wewe siku hizi unaongea kama sisi Waswahili, makubwa haya.“

„Usinitanie Josina, kwani zamani nilikuwa naongeaje?“

„Ilikuwa Kiswahili si Kiswahili, Kizungu si Kizungu, bali mchanganyiko maalum. Sasa naona msamiati wako umekuwa (vielleicht *umekua*), hata unadondoa misemo ya Waswahili.“

„Sasa naona umeamua kunitukana Josina!“

„Sivyo hivyo Peter, hii ni kweli lakini kweli inayouma. Hata hivyo tuyaache hayo. Peter, najua sana kuwa ulikuwa unanipenda na pengine bado unanipenda, lakini katika msingi ile ile ya bwana na mtumwa. Msimamo wangu unaujua Peter, si lazima nieleze tena.“

„Msimamo gani?“ Peter akauliza huku kakunja uso.

„Nilikueleza sana, pengine hukutaka tu kuelewa. Kwa ufupi, hayo pia tuyaache maana maji yaliyomwagika hayazoleki Peter. Vilevile mpanda ngazi na mshuka ngazi, kamwe hawashikani mikono,“ Josina akasema na kuelekeza macho baharini.

Kimya kidogo kikatoka. Peter akamwangalia Josina kwa muda, halafu akasema, „Nimekusikia Josina, lakini kabla sijaondoka nina maombi mawili. Kwanza, nieleze bila kuficha, nani aliyekushawishi mpaka mambo yetu yakatoka vile? Pili, wewe na Kalenga mna uhusiano gani?“ (Uk. 81-82)

Peter und Josina reden lange miteinander. Sie versucht ihm beizubringen, dass seine Eltern sie für die Tochter ihres Gärtners halten und nicht für eine Schwiegertochter aus ihrer Gesellschaftsschicht. Er aber verspricht ihr Liebe, eine gute Stelle in einem Amt, ein Auto, ein Haus und ein bequemes Leben. Ihre Ansichten sind aber so unterschiedlich, dass eine Ehe und ein Zusammenleben mit Peter für Josina nicht in Frage kommen. Sie lehnt seine Angebote höflich ab und sagt, „Mimi ni bwege.“ (Uk. 84). Er bietet ihr an, sie mit seinem Auto nach Hause zu bringen. Sie lehnt das Angebot dankend ab und geht zu Fuß.

Hamisi Mkela wohnt allein in Chang'ombe, ungefähr vier Kilometer vom Stadtzentrum Dar-es-Salaam entfernt. Kalenga ist bei ihm auf Besuch.

„Hii ni nyumba yako au ya Serikali?“ Kalenga akauliza huku akiikagua nyumba ya rafiki yake kwa macho.

„Ni yangu, niliinunua kutoka kwa mfanyabiashara mmoja hivi karibuni. Sikupenda nizoe kukaa bure kwenye nyumba za serikali, mazoea ya aina hiyo yana madhara yake,“ Hamisi akajibu huku anamwashiria Kalenga aketi.

„Kweli kabisa Hamisi, si mazoea mazuri hayo. Nyumba za serikali, licha ya fahari yake, hugeuka kuwa chungu mtu unapong'atuliwa. Lakini tajiri huyo hakukutoza fedha nyingi sana?“ Kalenga akauliza.

„Kwa kweli ni nyingi, shilingi laki moja. Ilibidi nipige bei gari langu nililokuja nalo kutoka Moscow.“

„Ulifanya vizuri Hamisi, maana nyumba ni muhimu zaidi ya gari. Kwanza mtu kuwa na gari katika hali ngumu ya uchumi kama hii ni sawa na kujinyonga.“

„Kwa kweli Kalenga, si rahisi kutunza gari katika nchi zinazoendelea,“ Hamisi akasema na kuelekea jikoni. (Uk. 86)

Kalenga und Hamisi plaudern über die Zeit, nachdem sie die St. Joseph's Secondary School in Dar-es-Salaam verlassen haben. Hamisi reiste nach Russland, um eine Ausbildung als Verkehrspilot zu absolvieren. In Moskau aber erfuhr er, dass er als Militärpilot ausgebildet werden soll.

Sie kommen nun zur Sache. Der Dienstwagen von Kalenga wurde gestohlen, als er sich im Büro des Ministers James Knox befand. Josinas Vater wurde die Bewilligung entzogen, sein kleines

Geschäft weiterzuführen. Es muss jemand dahinterstecken. Kalenga kommt auf den Strassenjungen Kitwana zu sprechen, der Erdnüsse verkauft. Kitwana bezeugt, dass die drei Männer, die Kalengas Dienstwagen abgeschleppt hatten, aus dem Auto von Mwapaker, dem Geschäftsführer der Firma Sufuria za Chai, gesehen wurden. James Knox und Mwapaker sind beide Mitglieder des Verwaltungsrates der Forodhani Secondary School.

„Ehe, kuhusu hao watu watatu, unasema Kitwana aliwaona kwenye gari la nani?“

„La Mwapaker.“

„Kwani huyo Mwapaker ana uhusiano wowote na Waziri James?“

„Sana. Kwanza, James na Mwapaker ni wakurugenzi wa Bodi ya Wadhamini ya Chuo cha Forodhani. Bodi hiyo nd'o iliyomwachisha kazi Josina, nadhani kutokana na athari ya Bwana James. Pili, James na Mwapaker ni marafiki wa siku nyingi mbali ya kwamba zamani walisoma shule pamoja. Hata wake zao wanatembeleana mara kwa mara. Vilevile, wana ushirikiano mkubwa katika kula milungura na biashara ya magendo, hasa usafirishaji wa vipusa nchi za jirani.“

„Usinishitue Kalenga, una hakika ya mambo haya?“ Hamisi akauliza.

„Si hakika tu, hata ushahidi ninao. Unamkumbuka Devkumar Puri, yule Baniani aliyekuwa anaishi Kinondoni sehemu ya Mwembe Jini, tuliyekuwa tukimsaidia kusukuma pikipiki yake karibu kila siku tulipokuwa watoto?“ Kalenga akauliza.

„Ndiyo namkumbuka, hivi bado yuko hai Mzee mla dengi yule?“ Hamisi akauliza.

„Ulidhani kesho kufa? Yuko hai na alishahama Kinondoni. Sasa ni jirani yangu pale katikati ya jiji.“ Kalenga akajibu. (Uk. 88)

Sie trinken ein Bier und plaudern gemütlich. Danach kommen sie wieder auf den Inder zu sprechen. Er wohnt im gleichen Gebäude wie Kalenga. Als Kalenga in diese Wohnung einzog, traf er ihn schon am ersten Tag im Stiegenhaus. Seither sind sie befreundet.

„Basi kwa ufupi hivi majuzi, Puri alikuwa kakerwa na tatizo fulani akashindwa hata kulala, akaja nyumbani kwangu kutafuta ushauri. Kwa kweli Hamisi kisa cha Puri kilinishangaza sana. Mwaka jana, Puri alimhonga afisa mmoja wa Benki ya Uchumi shilingi elfu saba ili ampitishie kwa haraka maombi yake ya leseni kuagiza bidhaa (*vielleicht*: kutoka kwa) nje ya nchi. Mambo yake yakafikia hatua za mwisho kabisa, lakini macho makali ya serikali yakawang'amua Puri na afisa huyo wa Benki wakatiwa ndani. Baada ya kukaa ndani kwa wiki moja hivi, wakaachiliwa kwa dhamana kwa vile Polisi walikosa ushaidi wa kutosha. Hata hivyo, upelelezi ukaendelea,“ Kalenga akaeleza, akawasha sigara ingine na kuanza kuvuta.

Hamisi alikuwa katulia kimya, anasikiliza kwa hamu kisa cha Baniani Puri. Kalenga akamweleza mwenziwe kuwa baada ya kushindwa kupata ushaidi wa kutosha, Polisi wakaitupia Bodi ya Kupunguza Milungura, kuendelea na upelelezi wa kesi hiyo.

„Nadhani unafahamu kuwa mkurugenzi wa bodi hiyo si mwingine bali *Sir Henry Mwapaker!* Basi, siku moja mnamo saa nne za usiku, Puri akashituka sana kufikiwa na mgeni aliyekuwa hamtazamii kabisa maishani *Sir Mwapaker!*“

Kalenga akazidi kueleza juu ya mkutano wa Puri na Mwapaker ulivyokuwa na jinsi ulivyomalizika kwa vitisho. Mwapaker alimtisha Puri kwa kumwambia kwamba bodi ilishapata ushaidi wote wa kesi yake ya rushwa, hivyo ajitayarisha kwa adhabu kali itakayotolewa na serikali.

„Alimpa Baniani yule jambajamba ya ajabu kwa kumwambia kuwa ushaidi huo ukipelekwa mahakamani, moja kwa moja atapata adhabu ya kifungo cha miaka kumi na kunyang'anywa leseni zake zote za biashara,“ Kalenga akaeleza. (Uk. 89-90)

Mwapaker verliess Puris Wohnung blitzartig. Hamisi ist neugierig zu wissen, wie die Sache weiterging.

„Kesho yake jioni, Mwapaker akafika kwa Puri na kutandaza mchezo mgumu sana. Puri akaambiwa atoe shilingi laki tatu na nusu ili faili la ushaidi lichomwe moto la sivyo faili hilo lisukumwe mbele kungojea uamuzi mkali wa Serikali. Puri hakuona njia nyingine, akakubali kutoa laki tatu u nusu hizo kusalimisha maisha yake,“ Kalenga akasimulia.

Baada ya kupata jibu hilo, Mwapaker akamtaka Puri azitoe fedha hizo kwa haraka sana, lakini asimkabidhi yeye. Akamtaka azipeleke nyumbani kwa Waziri James. Puri amenieleza kwamba alipeleka fedha hizo akidhani kuwa mambo yatakwish!“ (Uk. 90)

Hamisi und Kalenga trinken einen Schluck und schweigen nachdenklich eine Weile.

„Lakini Kalenga,“ Hamisi akauliza, „Nani aliyemweleza Puri nyumbani kwa James? Hakusindikizwa na mtu yeyote?“

„Hapana, aliongoza mwenyewe. Unajua Hamisi, hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa Puri kufika nyumbani kwa James. Puri anasema alikuwa anamfahamu James tangu mwaka juzi, wakati wa kashfa ya vipusa.“

„Kasfa ya vipusa! Nd'o ipi tena hiyo?“ Hamisi akauliza.

„Wewe ulikuwa Urusi wakati huo. Kashfa ya vipusa ni kisa kirefu sana ambacho kiliyumbisha nchi kwa zaidi ya miezi sita. Nitakuja kueleza marefu na mapana yake siku ingine (*vielleicht auch* nyingine), lakini kwa ufupi, kashfa hiyo iliwaumbua na kuwazika watu fulani na kuwanufaisha watu wengine,“ Kalenga akasema.

„Nifafanulie kidogo basi,“ Hamisi akambembeleza rafiki yake.

„Ni kwamba, kashfa hiyo ilipotokea, viongozi wengi walimwaga unga. Wachache ambao unga wao haukuguswa, wakateuliwa kuchunguza kashfa hiyo kwa undani zaidi. Nao walikuwa kina Knox James.

„Knox James, kama wenzake, akautumia vizuri uteuzi wake kwa kujipatia shibe, tena kwa njia za kishenzi sana.“

„Yaani kula, mwanya ukitokea,“ Hamisi akadakiza.

„Ewaa! Kwa mfano James na wenzake, waliwafuata watu wote waliohusika na kashfa hiyo, hasa wafanya biashara (*auch* wafanyabiashara) waliokuwa na ukwasi kama kina Puri. Ikawa si uchunguzi wala upelelezi tena, bali kashfa juu ya kashfa, milungura ya aibu hadi kwa mfano Puri akajikuta anamnunulia James gari jipya!“

„He!“ Hamisi akaonyesha mshangao.

„Ndiyo gari jipya! Unadhani ile *Audi Fox* mpya ya James kanunua nani? Ni Puri baada ya kutishwa na kufuatwafuatwa na James kwa muda mrefu. Si Puri tu, watu wengi waliokuwa na nafasi walitoboka mifuko kwa njia hizo hizo!“ Kalenga akaeleza na kujipapasa mifuko kwa njia hizo hizo. (Uk. 90-91)

Puri gab Knox das Geld und dieser leitete es an Mwapaker weiter. Hamisi glaubt alles, was Kalenga ihm diesbezüglich sagt. Er macht sich nicht einmal die Mühe, nach Beweisen zu fragen. Er geht im Zimmer auf und ab und stellt folgende Überlegung an.

„Mimi ningeweza kuingilia kati na kumtia ndani huyu Mwapaker. Lakini, kisheria itabidi na huyu Baniani nimfunge, kitu ambacho sipendi maana Puri kesho adhibiwa na kina Mwapaker,“ Hamisi akasema.

Kimya kirefu kidogo kikatokea, kila mmoja akijaribu kuwaza na kuwazua.

„Kalenga,“ Hamisi akaita na kukohoa kidogo, „miye napendekeza kuwa suala hili la Puri tusilikabili kwa pupa, tupeane muda kidogo kama siku mbili hivi tuweze kufikia jawabu imara. Unaonaje?“

„Naunga mkono mawazo yako, suala hili halihitaji papara hata kidogo,“ Kalenga akajibu. (Uk. 92)

Hamisi beauftragt rasch zwei junge Mitarbeiter, Mwapaker und James Knox zu beobachten. Auch der ehemalige Strassenverkäufer Kitwana soll eingebunden werden. Kalenga freut sich, dass sein Fall gute Aussichten haben wird. Er hat jedoch Angst um Hamisis Zukunft, denn Mwapaker und James Knox sind einflussreich. Danach kommen sie auf die Sekretärin von James Knox zu sprechen. Hamisi kennt sie. Sie war zusammen mit einer Sportmannschaft aus Tansania in Moskau. Dort hatte Hamisi sie kennengelernt. Sie heisst Blandina. Er dachte sogar an eine Verlobung in Moskau und an eine Hochzeit in Tansania nach der Rückkehr. Die beiderseitigen Eltern waren einverstanden. Es kam aber nicht dazu. Der Lebenswandel von Blandina entsprach seinen Vorstellungen nicht. Er bittet Kalenga um eine Möglichkeit, Josina kennen zu lernen. Kalenga möchte dies erst mit dieser besprechen. Kalenga verabschiedet sich und geht nach Hause. Dort wartet Kitwana auf ihn. Er hat das Abendessen zubereitet.

Das Telefon läutet beim Kamanda Mkuu Msaidizi Hamisi Mkela. Er ist im Begriff sich niederzulegen. Er steht auf und blickt auf die Uhr. Es ist 21 Uhr. Er ist müde und von den vielen langen Sitzungen zu Sicherheitsfragen erschöpft. Noch weitere Arbeit zu dieser Nachtstunde möchte er nicht haben. Trotzdem hebt er den Hörer ab. Kalenga ist am Apparat. Vorsichtshalber geht er zum Tresor, nimmt zwei Pistolen heraus und steckt sie in die Halter eines Kittels. Er fährt zu Kalengas Wohnung, der auf ihn wartet. Kalenga fürchtet, dass man Lauschwanzen in seiner Wohnung angebracht haben könnte. Sie gehen ins Disco Fever Haven zu Fuss.

Disco Fever Haven ilikuwa pepo kwa vijana. Kwa wazazi, ilikuwa kisima cha maovu walichokianguka kila siku kwa chuki, manung'uniko na wasiwasi mkubwa. Wasiwasi ulikuwa na msingi, maana Disco Fever Haven ilikuwa chambo chenye mnato mkali mithili ya ulimbo. Iliwanasa siku hadi siku vijana wa rangi mbalimbali, wafanyakazi, wahuni, vigoli, malaya, watoto wa shule na hata vikonge waliokuwa wakikataa umri wao, waliojulikana sana kuwa „wazee vijana“.

Kelele ya wazazi dhidi ya ukumbi huo wa starehe, ikawa kama petroli kwenye moto, Disco Fever Haven ikazidi kuvuma na kupotosha vijana wengi chini ya uongozi wa Boaz Kasongo, bepari uchwara aliyekuwa anaabudu neno moja tu duniani – fedha. Kasongo alikuwa na nafasi na sauti, kuku gani angeweza kumharibia biashara kwa malalamiko au manung'uniko? Hata hao waliokuwa wanalalamika walitambua wazi kuwa Kasongo alikuwa nguzo ya mawe – si ya mchanga – ya Disco Fever Haven.

Ukumbi ulikuwa umejaa kupindukia Kalenga na Hamisi walipoingia, wakaamua kujibanza upande wa kuume wa ukumbi huo. (Uk. 97)

Kalenga und Hamisi bestellen Bier und mishikaki (Fleischstücken am Röstspieß). Kalenga berichtet, dass er um 17 Uhr von Chefredakteur Ogola brieflich zu einer Sitzung eingeladen wurde. Kalenga fuhr sofort dorthin. Ogola erwartete ihn dringend. Im Büro fand sich eine hausfremde Person Mkurugenzi Mkuu wa Habari ya Taifa (Leiter des Staatlichen

Nachrichtendienstes) ein, Kuku Ndalama. Auch Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi (Sekretär des Verwaltungsrates) der Zeitung Kioo cha Bia war dort. Letzterer hielt eine lange Rede über Arbeitsdisziplin und durch verantwortliches Handeln der Journalisten dem „Kasumba ya maadui zetu“ (Uk. 99) zu entgehen. Danach kommt er auf Kalenga zu sprechen. Der Verwaltungsrat sei mit dessen Arbeitsdisziplin nicht zufrieden. Der Vorsitzende des Verwaltungsrates Tipis Ole Wankanye kommt dazu. Er entschuldigt sich wegen der Verspätung. Auch er ist mit Kalenga unzufrieden.

„Wakanye akaniangalia kwa dharau sana halafu akanieleza kuwa kwanza mimi nimeliletea gazeti aibu kwa kutiwa ndani, kwa sababu za ulevi. Akasema kuwa pili, mimi najifanya Mungu mdogo na wala sina heshima kwa viongozi. Kwa kuthibitisha hoja zake, aliendelea kusema ati zaidi ya viongozi kumi wamelalamika kwake kuhusu uchafu wa ulimi wangu. Tatu, akaniambia kuwa nimepoteza gari la ofisi lakini maelezo yangu hayakuridisha bodi,“ Kalenga akasema. (Uk. 99)

Kalenga verteidigt sich. Er sei nicht betrunken gewesen. Er könne nichts dafür, dass ihm das Dienstauto gestohlen wurde. Wakanye hat es eilig. Er übergibt Kalenga den Entlassungsbescheid und unterbricht die Sitzung, ohne sich zu verabschieden. Dem Bescheid zu Folge wird Kalenga entlassen, wenn er nicht innerhalb einer Woche das Auto ausfindig macht. Kalenga verlässt das Büro ohne Widerrede und geht nach Hause. Er zeigt Hamisi den Brief und bittet um dessen Rat. Hamisi legt ihm nahe zurückhaltend zu sein. Es ist schon spät nach Mitternacht. Beide gehen nach Hause.

Josina, Nuru und ihr Vater haben heute Onkel Binamu und dessen Frau Selina, die nach Mosambik zurückkehren, zum Flughafen begleitet.

Es ist spät am Abend. Josina geht zu ihrem Freund Kalenga. Sie ist arbeitslos und sucht nach Verdienstmöglichkeiten. Kalenga wartet vor dem Büro der Zeitung Kioo cha Bia auf sie .

„Nimechelewa?“ Josina akauliza huku anacheka bila sababu maalum.

„Hapana, umefika juu ya alama,“ Kalenga akajibu huku akiangalia saa yake ya mkono.

„Sasa, Hamisi yuku wapi? Uliniambia utakuwa naye,“ Josina akauliza.

„Suala la Hamisi ni ngumu kidogo. Nitakuelezea tukifika nyumbani. Si mbali kutoka hapa kwa miguu.“

Wakaanza kuhesabu hatua polepole bila kusema neno.

„Nakaa kwenye nyumba hiyo ndefu, orofa ya pili,“ Kalenga akaeleza walipokaribia.

„Eh! Kumbe uko Uhindini kabisa!“

„Siku hizi hakuna sehemu za Uhindini Josina, tumejitawala!“ Kalenga akasema huku akicheka.

„Utamdanganya nani. Weusi kama wewe ni wachache sana wanaoishi katikati ya jiji hili. Mfumo unaendelea kumpa Mhindi nafasi ile ile aliyokuwa nayo katika jamii zama za ukoloni.“

Kalenga akajibu kwa kicheko. Wakapanda ngazi za jumba hilo polepole, wakafika orofa ya pili na kubisha hodi.

Kitwana akafungua mlango na kuwaamkia. Wakaitikia na kuingia ndani. (Uk. 103)

Josina ist ausser sich vor Staunen, als sie die Wohnung sieht. Sie ist aber enttäuscht zu erfahren, dass die Wohnung der Firma gehört, bei der Kalenga angestellt ist. Dieser muss sie aber spätestens morgen räumen. Sie setzen sich und plaudern ein wenig. Sie möchte wissen, warum Hamisi nicht gekommen ist.

“Asubuhi ya leo niliongea na Hamisi kwa simu, akaahidi kuwa tutakuwa wote jioni hii. Lakini baada ya kurudi kutoka uwanja wa ndege kumsindikiza Binamu, nikampiga simu ofisini kwake, hakuwako. Nikajaribu simu ya nyumbani kwake, vilevile ikawa inaita tu bila kupokewa,” Kalenga akaeleza huku Josina anamsikiliza kwa makini.

Nikashikwa na wasiwasi. Nikampigia simu Kamanda Mkuu wa Polisi. Akanieleza kwa mkato na hasira kuwa Hamisi alikuwa amepata safari ya ghafla kwenda Uingereza,“ Kalenga akaeleza.

„Yaani sasa hivi hayuko nchini humu! Amewezaje kuondoka bila kuaga rafiki yake?“ Josina akauliza kwa mshangao.

„Hata miye nashangaa. Hamisi asingeweza kusafiri bila kunieleza. Nina shaka kuwa kuna kitu kinachohusiana na majanga yetu,“ Kalenga akasema.

Wakanyamaza kwa muda wa dakika tatu hivi. (Uk. 104)

Kalenga vermutet, dass der Kamanda Kuu wa Polisi (Polizeikommandant / Direktor) und Minister James Knox zusammenarbeiten. Sie werden herausgefunden haben, dass Kalenga und Hamisi miteinander befreundet sind. Die Parlamentswahlen stehen bevor. Minister James Knox kandidiert, muss aber gleichzeitig vor Gericht erscheinen. Vielleicht wurde Hamisi deshalb dienstlich ins Ausland entsandt. Kalenga teilt Josina seinen Geheimplan mit. Bis morgen wird der Chefredakteur von Kioo cha Bia dienstlich abwesend sein. Er möchte die Gelegenheit benützen, um Information über Korruption der „Oberen“ zu publizieren. Josina warnt Kalenga vor den Folgen, aber er bleibt bei seinem Vorhaben. Josina verabschiedet sich und fährt mit dem Bus nach Hause.

Kalenga geht zur Redaktion und berichtet den Mitarbeitern, dass nur Mzee Mkutane, Nsa und er die Nachtschicht bestreiten werden. Kalenga ist zurück in seiner Wohnung. Es läutet. Josina kommt herein. Sie ist heute besonders schön angezogen. Er ist unruhig. Er muss die Wohnung räumen und morgen ausziehen. Wohin er gehen soll, weiss er noch nicht. Josina ist um ihn besorgt. Sie weiß, dass es mehr als die Wohnung ist, was ihm Sorgen macht. Er lässt sie allein und geht sich waschen.

Baada ya dakika tano hivi, Kalenga akarejea na kuketi karibu sana na Josina.

„Mbona unanisogelea hivi na hali viti ni vingi hapa sebuleni,“ Josina akatania.

„Nataka unisikie vizuri,“ Kalenga akajibu.

„Ehe, nieleze basi, ulikuwa unawaza nini?“

„Kwa kweli sikuwa nawaza, nilikuwa najiuliza swali moja. Hivi wewe una mchumba?“

„Kwa nini unaniuliza?“ Josina akauliza huku amevaa mshangao zaidi usoni.

„Nijibu Josina,“ Kalenga akasisitiza.

„Jibu langu ni kwamba sina, sitaki na wala sijui kama nitakuwa naye.“

„Kwa nini?“ Kalenga akauliza.

„Kwa sababu ya mfumo. Hakuna thamani ya mapenzi siku hizi ni fedha, fedha, fedha tu. Wanaume wengi siku hizi ni waongo, wahuni na bado wanadhani kuoa ni kununua. Mimi najiona nina thamani zaidi ya fedha,“ Josina akasema.

Baada ya kimya kifupi, Josina akauliza, „Hivi kwa nini unaniuliza? Unafikiri nilimkataa yule kijana wa mashobo kwa ajili ya mwanamume mwingine?“

Kalenga akatingisha kichwa, „Hapana Josina, usinielewe vibaya, nilitaka tu kujua.“

„Na wewe je, una mchumba au rafiki wa kike?“ Josina akauliza huku akicheka.

„Sina.“

„Kwa nini?“ Josina akauliza tena.

„Nina sababu kama zako. Mfumo umechafua thamani ya mapenzi. Itabidi niwe na fedha au gari

kumpata mchumba na miye sitaki hivyo, ni kujidanganya,“ Kalenga akaeleza. (Uk. 114-115)

Beide verharren lange nachdenklich und schweigend. Josina starrt zur Decke, Kalenga zur Wand.

Mara Kalenga akaushika mkono wa Josina na kuanza kuuchezeachezea.

„Josina, Josina, nadhani nakupenda,“ Kalenga akapasua hisia zake kwa sauti ya kunong'ona.

„Unadhani unanipenda!“ Josina akajibu macho yake yakiwa bado darini.

„Dakika iliyopita nilidhani, sasa nakupenda Josina, nakupenda kwa dhati, nakupenda kwa moyo wote,“ Kalenga akasema huku anamsogelea zaidi Josina.

Josina hakusema kitu, akabaki akiangalia darini huku machozi yanamlengalenga. Kalenga akamshika Josina mabegani kwa uangalifu, „Mbona husemi Josina, mbona husemi?“

Bila kugeuza macho yake, Josina akatabasamu, „Niseme nini Kalenga, sielewi. Sielewi kwa nini unipende mimi maana nina matatizo mengi sana, nitakupaka nuksi.“

„Nuksi gani? Kama ni nuksi, wote tuna nuksi, miye nakupenda Josina!“ Kalenga akazidi kupasua hisia zake huku moyo wake ukidunda mithili ya ngoma.

„Josina ukikubali tuoane, nadhani matatizo yangu mengi yatapungua. Wewe ni pekee uliyejitokeza moyoni mwangu, nijibu Josina!“ Kalenga akalalamika kwa sauti ya unyonge. (Uk. 115)

Josina ist zurückhaltend. Ihr Leben ist voller Probleme, sie ist arbeitslos, das kleine Geschäft ihres Vaters ist zugesperrt, er hat kein Einkommen, Nuru geht noch zur Schule. Sie weiss auch nicht, was Minister James Knox mit ihr noch vorhat.

„Kalenga, nikikubali utanipa nini?“ Josina akauliza na kumwangalia machoni Kalenga ambaye alishitushwa kidogo na swali hilo.

„Nikupe nini Josina? Sina cha kukupa wala kukuahidi, ni mapenzi yangu tu,“ Kalenga akasema.

„Ni wewe niliyekuwa nakutafuta, Kalenga!“ Josina akasema na kumsongelea Kalenga.

Wakakumbatiana kwa nguvu na moto mkali wa mapenzi yaliyokuwa yamefukiwa kwa muda mrefu ukaripuka mithili ya volkeno. (Uk. 115-116)

Mzee James überkommt kalter Schweiss, während seine Frau in der Wohnung herumirrt, wie ein Schaf, das seinem Hirten sucht.

Gazeti la *Kioo cha Bia* lilikuwa mezani likiwaangalia bibi na bwana kwa kebehi kubwa. Mtoto wao Peter ambaye alikuwa hajaonekana nyumbani usiku mzima, akazidisha moto wa jambajamba katika nyumba ya James.

Mitaani, umati kubwa wa watu ulikuwa ukigombania magazeti machache yaliyokuwa yamebaki madukani, hata makonde yakaumuka katika pata-shika hizo. Vikundi vikubwa vya watu vikaonekana vikijikusanya barabarani kusoma gazeti moja. Alimradi, likawa zogo la ajabu mjini.

„Hawapati kura yangu hawa! Kumbe siku zote wamekuwa wakitulaghai kama watoto wadogo,“ Mzee mmoja akasema huku kashikilia nakala moja ya gazeti la *Kioo cha Bia* kwenye kituo cha basi.

„Wapelekwe mahakamani hawa!“ Abiria wengine waliokuwa walingojea mabasi kwa hamu wakafoka.

„Kwa nini tuwacheleweshe, tuwanyang'anye mali waliyotuibia halafu wapigwe vichwa tu!“ Kijana mmoja mrefu na mwembamba mithili ya mwanzi akatamka kwa hasira. Alimradi ilikuwa hekaheka kutwa miongoni mwa wakazi wa mjini. Nyumbani kwa Mzee James, safari za kwenda chooni zikazidi maradufu, ikiwa si kuharisha tena bila kuhara.

„Ni kijana yuleyule mke wangu, aliyeniumbua kwa kunipeleka makahamani ambaye leo kaandika makala zote hizi ili kuniumbua zaidi. Ni huyo kijana Kalenga na yule mtoto malaya wa Simango ambao wameamua kutuumbua kadamnasi ya watu!“ Mzee James akalalamika kwa mkewe bila kituo huku akikimbilia msalani.

Nyumbani kwa Simango, Josina alikuwa kajifungua chumbani kwake alitambua kuwa wakati wowote ule askari wangemjia na kumtia kizuizini. (Uk. 117)

Josina erinnert sich an die Ereignisse der vergangenen Nacht. Als Kalenga und sie zur Druckerei unterwegs waren, hielt ein Auto der Type Audi Fox plötzlich vor ihnen an.

Akateremka Peter James na kuwasalimu kwa kebehi.

„Josina, kumbe huyo mwongo nd'o Bwana wako!“ Peter akasema kwa sauti kali.

„Mwongo baba'ako, usimtanie mume wangu,“ Josina akajibu kwa ukali. Kalenga akamkataza Josina asiseme kitu.

„*Stupid, shut up.* Nitakutia vibao sasa hivi Josina! Wewe mbwa mkubwa Kalenga, mimi nakuona kama *shit* tu. Jitayarishe, kesho au kesho kutwa wewe utakuwa gerezani, tutakusahau huko kwa sababu ya mdomo wako mchafu.

„Halafu nani amekuruhusu kutembea na Josina? Unatambua kuwa Josina bado ni mke wangu kisheria!“ Peter akabwata akionyesha kuwa alikuwa kalewa chakari.

Kalenga hakujibu kitu. Akamshika mkono Josina na kurejea walikotoka.

„Leo nitakufa mimi, Josina au wewe Kalenga. Sikubali hata kidogo mbwa kama wewe uende na Josina; ni *wife* wangu huyo utake usitake,“ Peter akafoka huku povu linamtoka kinywani.

Peter akaingia garini na kumwamrisha dereva wake awafuate kina Kalenga ambao walikuwa wameshatokomea gizani.

Kalenga na Josina hawakwenda mbali, wakajibanza upenuni mwa nyumba moja huku wakichungulia Peter.

Wakaliona gari la Peter likifuata njia yao, likawapita na kutokomea gizani. (Uk. 118)

Sie beeilen sich in die Druckerei, wo Nsa und Mkutane auf sie warten. Um Mitternacht ist die Zeitung bereits gedruckt. Die Firma Kampuni ya Wasambazaji Magazeti holt die Auflage zur Verteilung ab. Josina geht nach Hause und Kalenga zieht während der Nacht mit einem gemieteten Auto in seine neue Wohnung in Manzese um, übernachtet aber bei seinem Vater.

In der Wohnung von Mzee James Knox herrscht Stille. Er hält sich am Dachboden versteckt. Seine Frau soll Besuchern mitteilen, dass er verreist sei. Peter ist nicht nach Hause gekommen. Der Hausdiener kommt nicht mehr zur Arbeit. Die Frau von James Knox hört ein Auto vorfahren. Sie freut sich, da sie meint, Peter sei nach Hause zurückgekehrt. Es ist aber nicht Peter, sondern der Chauffeur Fung'o.

„Shikamoo Mzee, shikamo Mama,“ Fung'o akawasabahi. Wakaitikia kwa unyonge na kumkaribisha kitini.

„Mzee nimekuja kukuchukua ili uwahi kwenye shughuli za kampeni,“ akaeleza Fung'o baada ya kuketi. Mzee James hakujibu kitu, akabaki kumwangukia mkewe.

„Hivi umemwona Peter mjini?“ Mama Peter akadakiza.

„Kwa leo hapana. Ila jana nilikuwa naye kwa muda mrefu,“ Fung'o akajibu.

„Ulikuwa naye wapi?“ Mama Peter akauliza akionyesha shauku kuu.

„Mjini. Nilipomaliza kazi jana jioni, nikaenda moja kwa moja nyumbani kwangu kupumzika. Mnamo saa moja na nusu hivi jioni, Peter akafika nyumbani kwangu na lile gari *Audi Fox*. Akaniomba nimwendeshe maana alikuwa kalewa sana,“ Fung'o akaeleza.

„Ehe, hebu endelea kueleza,“ Mama Peter akasema.

„Mimi nikakubali. Nikamwendesha hadi saa sita ya usiku. Nilipomwambia nimrudishe nyumbani akalale, akakasirika na kuninyang'anya funguo za gari. Sielewi alielekea wapi,“ Fung'o akaeleza. Mzee James na mkewe wakapigwa na butaa zaidi. Haikuwa kawaida ya mtoto kulala nje au kulewa kupita kiasi.

„Fung'o, hivi hakukudokezea hata kidogo mahali alikokuwa anataka kwenda?“ Mama Peter akauliza zaidi.

„Hapana Mama, hakunieleza. Ila tu, alisema anamtafuta msichana mmoja anaitwa ..., anaitwa Josina ambaye mnamo saa mbili hivi ya usiku tulikutana naye barabarani akiwa na mwandishi mmoja wa habari wa *Kioo cha Bia*,“ Fung'o akasema huku Bwana na Bibi James wakitupiana macho kwa wasiwasi.

„Makubwa haya jamani,“ Mama Peter akalia, „alikuwa akimtafuta nini malaya huyo?“

„Mama, nafikiri Peter alikuwa kalewa sana maana alitaka hata kupigana na kijana aliyekuwa na msichana huyo. Peter aliniambia kuwa msichana huyo ni mke wake na akaapa kuwa hataridhika mpaka apambane nao,“ Fung'o akaeleza.

„Sasa kwa nini ukamwacha Peter katika hali kama ile?“ Mama Peter akamlaumu Fung'o.

„Mama, mimi sikutaka kumwacha Peter hata kidogo. Ila yeye alininyang'anya funguo za gari, halafu akanitupa nje na kuondoka kwa kasi sana,“ Fung'o akajitetea.

Kimya cha kutisha kikaifunika nyumba ya Mzee James. Mama Peter akajishika tama akiwaza juu ya mwanawe. Bwana na Bibi James, walikuwa na mtoto mmoja tu, Peter. Mzee James akanyanyuka kitini polepole na kuelekea msalani. Baada ya muda mfupi, akarejea na kumwamuru dereva aondoke.

„Kijana, nenda nyumbani, mimi siendi kwenye kampeni,“ akasema na kumgeukia mkewe, „tufanye nini mke wangu, naona kila kitu sasa kinakwenda mrama.“ (Uk. 120-121).

Seine Frau rät Minister James, Mwapaker anzurufen. Mwapakers Frau teilt Minister James mit, dass Mwapaker derzeit nicht erreichbar sei. Die Polizei hat auf Grund eines Berichts der Zeitung Kioo cha Bia viermal das Haus durchsucht. Mwapaker haben sie aber nicht gefunden.

Es läutet bei Minister James Knox. Drei Polizisten treten ein, geführt von einem jungen Offizier.

„Mzee James, sasa hivi uko chini ya ulinzi wa Polisi. Tunaondoka nawe sasa hivi kwenda kituo cha Polisi,“ kijana huyo aliyejitambulisha kuwa Kamanda Mkuu Msaidizi wa Polisi, Hamisi Mkela aliamuru huku amenuna.

Mama Peter akaanguka kilio kikali mithili ya king'ora cha moto na kuzirai.

„Naomba nielewe niko chini ya ulinzi kwa sababu gani?“ Mzee James akataka kujua.

„Utalewa mbele ya safari, twende ndugu usitupotezee muda,“ Kamanda Hamisi akasema huku anamsukuma Mzee James.

„Kijana lazima utambue kuwa mimi ni Waziri, huwezi kunisukuma kama mwizi wa sokoni. Vilevile lazima nielewe kwa nini niko chini ya ulinzi. Je, ni kwa sababu ya upuuzi ulioandikwa

gazetini humu?“ Mzee James akajitutumua.

„Lazima na wewe utambue kuwa mimi ni Kamanda wa Polisi na niko kazini. Nikitoe amri lazima uifuute. Suala lako halihusu makala zote zilizoandikwa humu gazetini. Ni makala moja tu ndogo inayotuhusu sisi Wana-Usalama na wewe! Makala zingine zinakuhusu wewe na umma uliokuchagua, si Polisi,“ Kamanda akasema kwa sauti ya madaraka.

„Mbona sikuelewi?“ Mzee James akazidisha ubishi. (Uk. 122)

Minister James Knox versucht, den Polizei-Kommandanten in ein Gespräch zu verwickeln. Der Kommandant Hamisi Mkela bleibt aber hart.

Kamanda Hamisi akatoa gazeti la *Kioo cha Bia* mfukoni mwake na kufungua ukurasa wa katikati. Akamwonyesha habari moja fupi iliyokuwa imeandikwa chini ya kichwa cha habari, „KIONGOZI ANAIUZA NCHI KWA MAKABURU.“

Mzee James macho yakamtoka pima. Alikuwa hajaisoma habari hiyo. Yeye tangu asubuhi, macho yake yalikuwa ukurasa wa mbele wa gazeti wala hakufungua ndani kusoma habari zingine. Akaisoma habari hiyo huku machozi yanamlengalenga. Jina la kijana aliyeiandika habari hiyo lilikuwapo na alikuwa analifahamu sana ... Kalenga Mabruki (Kamarada K.)

Ilikuwa habari fupi lakini nzito yenye uchambuzi na uchunguzi wa hali ya juu. Ilikuwa inaeleza kwa muhtasari uhusiano wa hatari kwa nchi uliokuwapo kati ya Mzee James, *Sir Henry Mwapaker* na jasusi mmoja wa kikaburu, *Botha Piet Botha* ambaye alikuwa anatafutwa karibu kila nchi ya Kiafrika.

„Uhusiano huu, hata uwe wa kibiashara tu, ni hatari kwa mapinduzi na usalama wa nchi yetu. Mtu yeyote, awe kiongozi au raia, mwenye uhusiano wa aina yoyote na nyoka kama huyu ambaye ameua maelfu ya Waafrika huko Afrika ya Kusini, ni msaliti na haini mkuu wa Bara la Afrika na Taifa letu,“ habari hiyo fupi ikasema.

Chini ya habari hiyo, kulikuwa na picha ndogo ya Mzee James, *Sir Henry* na jasusi *Botha*, walipokuwa katika mazungumzo nyuma ya Hoteli ya Amana usiku wa manane.

Mzee James akapigwa na butaa, akafunua mdomo ili aseme kitu, akashindwa.

„Maelezo mengine utayapata Polisi, haya twende!“ Kamanda Hamisi akasema kwa sauti kali. (Uk. 122-123)

Kamanda Hamisi Mkela fordert Minister James Knox auf, ihm sofort auf die Polizeistation zu folgen. Kamanda Mkela beauftragt den Polizisten Mchapo, im Haus zu bleiben und der Frau des Ministers beizustehen, bis sie wieder zu sich kommt und sich erholt.

Kalenga liest weiter in der Zeitung Kioo cha Bia. Er denkt zurück an jene Nacht, in der Mkela und er James Knox und Botha beobachtet haben. Schließlich um ungefähr zwei Uhr in der Früh erspähten sie James Knox, Mwapaker und Botha in der Umgebung des Amana Hotels, wie sie dort Aktenkoffer ausgetauscht haben. Kalenga und Mkela verfolgen Botha bis ins Kilimanjaro Hotel, wo dieser wohnt, und legen ihm Handschellen an. Er wird verhört. Es stellt sich, dass der Aktenkoffer Informationsmaterial über den Befreiungskampf in Südafrika enthielt, den Tansania unterstützt. James Knox wird dafür honoriert. Botha und Knox trafen sich einmal im Jahr. Botha wird in ein Hochsicherheitsgefängnis gebracht.

Ein anderer Artikel in der Zeitung berichtet über Kashfa ya Vipusa. In allen Einzelheiten wird dort berichtet, wie James Knox sich ein neues Auto von einem Inder namens Devkumar Puri schenken ließ, als Gegenleistung für Begünstigungen im Geschäftsbereich. Henry Mwapaker war der Vorsitzende der Bodi ya Kupunguza Milingura, arbeitete privat jedoch in einem ganz

anderen Sinn.

Im Hause Kalengas herrscht Sorge. James Knox hat dem Vater die Bewilligung entzogen, ein Geschäft zu führen. Kalenga ist arbeitslos, seine Mutter macht sich Sorgen um ihn. Plötzlich stehen vier Polizisten in Begleitung von Bubu Oyola vor der Tür. Einer von ihnen, Inspektor Kiboko Maskini, fragt Kalenga nach seiner Identität. Er wird festgenommen. Er verabschiedet sich von seinen Eltern mit den Worten:

„Wazee msilie, msinionee huruma wala kunilaumu. Niliamua mimi mwenyewe na malipo yake niliyotazamia nd'o haya. Kwaherini!“ (Uk. 125)

Das Polizeiauto fährt jedoch nicht zur Polizeistation, sondern zum Wizara ya Siasa na Usalama wa Nchi (Ministerium für Politik und Staatssicherheit). Alle steigen aus und gehen zum Büro des Ministers. Die Handschellen werden Kalenga abgenommen. Er wird dem Minister vorgeführt.

Ofisi hiyo ilikuwa kubwa na nzuri sana. Nyuma ya meza moja ya kioo, aliketi Mzee aliyekuwa anamfahamu sana, Dk. Chenza Karl Chenza. Kalenga na Inspekta Maskini walipoingia walimkuta Dk. Chenza akainua macho na kumwona Kalenga, akatabasamu na kumwashiria aketi. Moyo wa Kalenga ukatuta kwa kasi zaidi alipoliona gazeti la *Kioo cha Bia* juu ya meza ya Waziri.

„Wewe ndiye Kalenga Mabruki? Inakuwa kama tumewahi kukutana mahali fulani,“ Dr. Chenza akasema kwa sauti nzito.

„Ni kweli Mzee, tulikutana Msumbiji mwaka juzi ulipofika kwa ziara ya kiserikali,“ Kalenga akasema.

Waziri akatabasamu huku akitingisha kichwa, halafu kwa ghafla akanuna.

„Eee, kijana nimekuita hapa kwa ajili ya suala zito la kitaifa. Leo hii asubuhi, nilikuwa nakutana na viongozi wenzangu. Tumejadili kwa urefu sana mambo yaliyotokea leo ambayo wewe ni chanzo chake,“ Waziri akakohoa kidogo na kujipapasa mifukoni. (Uk. 126)

Dr. Chenza zieht eine Schachtel Zigaretten aus der Hemdtasche und steckt sich eine an. Er bietet Kalenga eine Zigarette an, dieser lehnt dankend ab. Er setzt das Gespräch fort.

„Kijana, jambo ulilofanya si dogo, ni kubwa ambalo linaweza kuhatarisha sana usalama wa nchi. Kosa lako kubwa ni kuwa hukufuata taratibu zilizowekwa na Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyokuwa yanakukabili,“ Waziri akaeleza.

„Mkutano wetu wa leo, umeamua mambo manne makubwa na inabidi utege sikio vizuri,“ Waziri akasema halafu akanyamaza.

„Kwanza,“ Waziri akaendelea baada ya kimya kifupi, „hoja nyingi zilizotolewa wakati wa mkutano wetu mojawapo ilikuwa kukuadhibu vikali sana,“ Waziri akaeleza huku Kalenga akizidi kulowana kwa jasho la kukata tamaa.

„Hoja hiyo kijana, wengi tulikataa maana unapomwadhibu mtu lazima iwepo sababu ya msingi. Vilevile, adhabu lazima iwe na lengo la kumnyoosha mtu. Wewe umekosa, lakini katika kukosa kwako umeweza kuanika hadharani kweli fulani, kweli ambayo ni zito zaidi ya kosa lako. Hivyo mkutano wetu leo umeniomba nikupe onyo kali sana kuwa njia uliyoitumia si nzuri hata kidogo. Nchi yetu ina demokrasi ya kimapinduzi kabisa. Baada ya kuona yote hayo uliyoyaandika, usingelikimbilia kuyatangaza gazetini, ungekuja kwangu au kiongozi yeyote kufuatana na utaratibu iliowekwa na Serikali,“ Waziri akasema na kunyamaza tena. (Uk. 127)

Die Stimmung ist gespannt. Ein Paar Augenblicke herrscht Stille. Dann trägt Dr. Chenza den zweiten Beschluss vor.

Baada ya kimya kifupi, Dk. Chenza akaendelea, „Pili, mkutano uliona kuwa pengine kwa sababu ya ugeni wako na mfululizo wa majanga uliyoyapata, hukuweza kuamini kuwa malalamiko yako yangelisikilizwa vilivyoo. Kutokana na mtazamo huu, mkutano umeamua kukupongeza kwa moyo wako wa uzalendo na ujasiri. Umefichua uozo wa ajabu uliokuwa umefichika kwa muda mrefu sana katika jamii yetu,“ Dk. Chenza akasema. (Uk. 127)

Der dritte Beschluss folgt.

„Tatu, mkutano wetu wa dharura, umekupongeza sana kwa moyo wako wa kutetea na kuimarisha siasa yetu ya kimapinduzi. Vilevile, mkutano umefurahishwa sana na taarifa yako kuhusu jasusi Botha ambaye nchi zote za kimapinduzi zinamtafuta bila mafanikio. (Uk. 127)

Es folgt der vierte.

„Nne na mwisho, tumeamua kukupa madaraka ya kuliongoza gazeti la *Kioo cha Bia* katika ngazi ya Mhariri Mkuu kuanzia dakika hii. Tuna matumaini kuwa gazeti lako litakuwa mstari wa mbele katika kujenga na si kubomoa maadili ya siasa ya nchi,“ Waziri akasema na kumkabidhi Kalenga barua ya kupandisha cheo kuwa Mhariri Mkuu. Waziri akasimama na kumpa Kalenga mkono wa pongezi. Inspekta Maskini, akiwa kapigwa na butaa, vilevile akasogea na kumpa Kalenga mkono wa hongera. (Uk. 127)

Kalenga kann es kaum fassen. Ihm wird schwindlig. Er steht trotzdem stramm, dankt dem Minister für die Beförderung und verspricht, aus der Zeitschrift nicht nur einen „Spiegel“ (Kioo), sondern eine „Fackel“ (Mwenge) zu machen. Der Minister beauftragt ihn, sofort an die Arbeit zu gehen. Inspektor Maskini bietet Kalenga an, entweder zu den Eltern oder ins Büro zu fahren. Kalenga möchte zuerst zu seine Eltern sehen und ihnen die gute Nachricht mitteilen, noch früher möchte er aber Josina kurz besuchen. Sie fahren mit dem Polizeiwagen zu ihr, bleiben aber in einiger Entfernung stehen. Zwei Polizeiwagen, eine Ambulanz und ein Auto stehen nun vor dem Elternhaus Josinas.

Kalenga akaliangalia gari hilo aina ya *Audi Fox* kwa wasiwasi sana. Akateremka kutoka gari la Polisi kwa haraka na kuingia ndani ya nyumba huku Inspekta Maskini akimfuata kwa kasi. Mwili wa Kalenga ukasisimika alipoona watu watatu wamelazwa sebuleni wakiwa wamefunikwa gubigubi kwa mashuka meupe.

Akauangalia umati wa watu uliokuwa umejazana sebuleni. Kalenga akashangaa kidogo kumwona rafiki yake Hamisi upande wa kiume wa sebule. Hamisi alikuwa akiongea na Komba na Nuru ambao macho yao yalikuwa na yamevimba kwa kulia sana.

„Kuna nini jamani, kuna nini niambieni!“ Kalenga akalia.

Hamisi akaacha kuongea na kina Komba na kumkimbilia rafiki yake. Akamshika mkono na kumvutia pembeni.

„Sikiliza, Kalenga, lazima uwe na moyo wa kijasiri. Ukilia wewe mtu mzima, je huyo mtoto mdogo atafanya nini?“ Hamisi akasema huku akinyoosha kidole kwa Nuru.

Basi Hamisi niambie kumetokea nini. Kwani Josina yuko wapi?“ Kalenga akauliza huku machozi yanamlengalenga.

„Jikaze Kalenga, nakuomba jikaze. Kwa ufupi, Mzee Simango, Peter mtoto wa James na Josina

wamekufa!“ Hamisi akaeleza.

Mshale mkali wa simanzi ukapenya moyoni mwa Kalenga. Kizunguzungu kisicho cha kawaida kikamkumba, akayumba mithili ya mlevi na kuanguka sakafuni kwa mshindo mkubwa, akazirai. (Uk. 128-129)

Es ist ganz dunkel, als Kalenga im Hause Simangos das Bewusstsein wieder erlangt. Er betastet die Matte, auf der er liegt. Sie ist ganz nass. Er weiss nicht, ob er träumt, oder ob er die Welt bewusst wahrnimmt. „Ist Josina wirklich gestorben?“ fragt er sich. Er sitzt aufrecht auf der Matte und hebt den Kopf. Er kann seinen Augen kaum glauben. Viele Leute haben sich im Hof versammelt. Als er im Begriff ist, zu stürzen, hält ihn eine Hand fest. Es ist die Hand Hamisi Mkelas. Er weist Inspektor Maskini an, Nuru zunächst in seine (Mkelas) private Wohnung in Chang'ombe zu bringen. Kalenga bietet ihr an, vorübergehend bei ihm zusammen mit Kitwana zu wohnen. Sie stimmt zu.

Baada ya kimya cha muda mfupi, Kalenga akamwona Hamisi amwelezee kwa ufupi kuhusu maafa yalivyotokea.

„Peter, mtoto wa James, ndiye aliyemuua Josina,“ Hamisi akaeleza huku akiangalia chini.

„Inasemekana kuwa jana usiku, Peter alikuona na Josina mjini, akathibitisha mashaka yake kuwa wewe na Josina mlikuwa kweli mmepegangia kuoana.

„Suala la kuoana wewe na Josina lilikuwa kisu kikali moyoni mwa Peter kwa sababu kuu nne kufuatana na uchambuzi uliofanywa na Polisi leo mchana.“

„Kwanza, akili ya Peter ilikuwa imeharibika kidogo kutokana na pigo la kukataliwa kanisani na Josina. Hivyo, alitaka Josina afe au azeeke bila kuolewa na mtu mwingine yeyote.“

„Pili, Peter alikuwa bado akimpenda sana Josina ingawa alijua waziwazi kuwa yeye alikuwa hapendwi. Hivyo, hakutaka mtu yeyote amsogelee Josina, ambaye bado alikuwa anampenda sana moyoni.“

„Tatu,“ Hamisi akaendelea kueleza, „Peter alikuwa anakuchukia sana Kalenga kwa sababu mbalimbali ambazo nyingi unazijua.

„Hivyo alikuwa daima akikuona kuwa adui wake na wa familia yao. Sasa alipohisi kuwa wewe ulikuwa na nia ya kuoana na Josina, uadui wake kwako ukakua, akala yamini ya mapambano, afe yeye, Josina na wewe, alimradi usimpate Josina.

„Nne, inaaminika kuwa Peter alikuwa kalewa sana kwa fikra za kitabaka. Kwa vile yeye alijiona mtu wa juu, hakuwa radhi kumwona mtu duni kama wewe unamwoa Josina, msichana aliyemkataa. Hivyo akaamua kuendeleza mapambano ya kufa na kupona,“ Hamisi akaeleza. (Uk. 131-132)

Hamisi Mkela denkt einen Augenblick nach.

Baada ya kukohoa kidogo, Hamisi akaendelea, „kufuatana na ripoti ya Polisi, Peter alikutafuta sana jana usiku baada ya kukuona na Josina. Aliposhindwa kukupata, anasemekana alilala kwenye gari karibu na hoteli ya Amana. Kufuatana na ushaidi wa watu mbalimbali, Peter alikuja kuzinduka usingizini mnamo saa sita ya mchana ya leo. Akaenda hoteli ya Amana, akaoga na kupumzika kidogo.

„Watu wengi wameeleza kuwa muda wote aliokuwapo hotelini, alikuwa akiuliza nyumbani kwako. Hatimaye akaonyeshwa na mlinzi wa hoteli hiyo, sielewi aliifahamuje.“

„Peter akafika nyumbani kwako, lakini hakukuta kitu. Akaamua kumfuata Josina. Inasemekana kuwa gazeti la leo liliongeza chuki yake kwako, akaamua kutimiza kiapo chake. Akaja moja kwa moja mpaka hapa nyumbani, lakini hakumkuta mtu. Simango na Komba walikuwa mjini kwenye

shughuli za kampeni na Nuru wakati huo alikuwa akicheza na watoto wa jirani yao, Mama Tabu.“

„Peter akakagua nyumba nzima bila kuona mtu. Akafungua chumba cha Josina, akamkuta kalala fofofo. Kilichotokea hapo, kwa kweli hatuna habari kabisa ila tu majirani walisikia milio ya bastola. Majirani walipokurupuka kuja kuona kilichotokea, wakakuta Josina amekufa baada ya kupigwa risasi ya kichwa na Peter akipigapiga mateke ya mwisho baada ya kujipiga risasi ya kifuani.“ (Uk. 132)

Komba berichtet der Polizei, überall seien die Berichte Kalengas zur Korruption in Kioo cha Bia diskutiert worden, während er und Simango in der Stadt waren. Sie wollten daher rasch nach Hause zurückkehren und mit Josina sprechen, da diese an der Veröffentlichung beteiligt war. Sie waren überrascht, eine so grosse Menge vor dem Haus vorzufinden.

„Kufuatana na maelezo ya daktari, Mzee Simango alipouona mwili wa binti yake umetapaka damu, akapata papo la moyo, akamwangukia binti yake na kukata roho papo hapo,“ Hamisi akamaliza maelezo yake na kumwangukia Kalenga. (Uk. 133)

Kalenga hört aufmerksam zu und schweigt. Hamisi Mkela ermuntert ihn, stark zu bleiben und durchzuhalten. Kalenga erkundigt sich nach James Knox und Henry Mwapaker. Hamisi teilt ihm mit, dass beide in Untersuchungshaft sind. Ihnen wird Landesverrat (uhaini), Entwendung von Volkseigentum (wizi wa mali ya umma) und Korruption (rushwa) vorgeworfen. Kalenga wünscht noch einen Blick auf Josinas Leiche werfen zu dürfen. Er spricht ein Abschiedswort.

„Josina, nitaendelea kukupenda na kukukumbuka daima. Josina nilikupenda sana Josina. Josi ... Josina, naahidi kuwa nitamwangukia Nuru kwa mapenzi yote. Nitamtunza kama dada yangu wa tumbo moja. Josina. Josina. Josi ...,“ Kalenga akalia bila kituo.

Hamisi akashikwa na huruma, akamwinua rafiki yake na kuufunika mwili wa Josina. Akatoa amri kwa askari kuzipeleka maiti hospitali. (Uk. 133)

Kalenga wohnt schon drei Tage in der Dienstwohnung des Chefredakteurs der Zeitung Kioo cha Bia. Mitternacht ist vorüber. Nuru und Kitwana schlafen. Das Telefon läutet. Kalenga geht und hebt den Hörer ab. Hamisi ist am Apparat. Kalenga macht sich Sorgen. Am Josinas Sterbetag sah Hamisi sehr verstört aus. Er war sehr schweigsam. Er hatte Kalenga ersucht, ihn nicht anzurufen. Kalenga zieht sich an, steigt ins Auto und fährt zum Hotel Misakato, so wie Hamisi es angeordnet hat. Nach zehn Minuten ist er schon do. Er sieht Hamisi, der sich unter einem grossen Mangobaum vor dem Hotel versteckt hält. Hamisi gibt Kalenga ein Zeichen, dass er rasch ins Hotel gehen soll. Nach einigen Minuten stürmt Hamisi herein. Er nimmt Kalenga bei der Hand und führt ihn in ein kleines Zimmer nahe der Toilette. Dort gibt es einen Tisch, einen Telefonapparat und ein Bett.

„Kalenga, usishangae Ndugu yangu,“ Hamisi akasema baada ya kuketi kwenye kitanda. Kalenga alikuwa ameketi kwenye kiti cha mbao akiangaliana na Hamisi.

„Nimekuita wakati huu wa usiku ili nikuume sikio uweze kuielewa hali halisi inayonikabili mimi nduguyo.

„Nimekuita ili uje uwe shaidi ikiwa leo, kesho au kesho kutwa nitauawa,“ Hamisi akasema kwa sauti ya chini.

Kalenga akashikwa na hofu, akamwangukia Hamisi kwa wasiwasi. Hamisi alikuwa amekonda kidogo. Juu ya meza hiyo yenye tarizi za Kiarabu, kulikuwa na bunduki moja kubwa na bastola

mbili. Kalenga akaziangalia silaha hizo kwa jicho la hofu.

„Tangu tuonane juzi, nduguyo nimekuwa windo kubwa la askari wenzangu. Hadi dakika hii, nimekoswa-koswa risasi zaidi ya mara kumi.“

„Lakini kwa nini?“ Kalenga akauliza kwa hasira.

„Nitakuelezea. Si unakumbuka kuwa hivi karibuni nilipewa safari moja ya ghafla? Basi safari hiyo ilikuwa mbinu ya wakubwa fulani kutaka kuniua. Nitakuelezea sababu yake. Tulipomkamata jasusi Botha hivi karibuni, sikutaka wakuu wangu wa kazi wajue maana nilikuwa na mashaka fulani kuwa wangeniharibia mipango yangu ya upelelezi.“

„Waliokuwa wanafahamu kuhusu jasusi Botha ni vijana wangu wawili tu ninaowaamini sana, Inspekta Maskini na Inspekta Mwaikusa, nd'o vijana waliokuwa wanaendesha upelelezi wa kesi yako. Maskini na Mwaikusa nd'o pekee katika jeshi letu waliokuwa wanaifahamu siri hiyo. Nikawapa hata madaraka ya kumlinda huyo jasusi ili tu habari hiyo isienee,“ Hamisi akaeleza na kukohoa kidogo.

„Nilipopewa safari hiyo ya ghafla, nikasita kidogo maana sikuona umuhimu wake. Ati kwenda Ufaransa kuulizia kuhusu ripoti ya mwaka ya Shirika la Polisi la Kimataifa, INTERPOL. Mimi nikamweleza Kamanda wangu mkuu ripoti hiyo ingeweza kupatikana hata kwa kuandika barua tu, lakini akasema yeye aniamuru niondoke haraka iwezekanavyo.“

„Lakini kabla sijaondoka, vijana wangu hao wakanifuata usiku nyumbani kwangu na kuniambia kwamba kulikuwa na mpango wa kuniua nifikika Ufaransa. Wakanishauri kuwa safari yangu iishie Nairobi.“ (Uk. 134-135)

Hamisi Mkela ist nicht nach Frankreich geflogen, er blieb in Nairobi. Einen ganzen Tag verbrachte er in Muße und spazierte in der Stadt herum. Er kam auf den Gedanken, einen gewissen McDonald aufzusuchen, der Bothas Auftraggeber war. Hamisi suchte die Polizeidirektion von Kenia auf und berichtete von der Festnahme des Spions Botha. Es folgte die Suche nach McDonald, die schon nach einigen Tagen erfolgreich war. McDonald wurde festgenommen und eingesperrt. Er stand unter dem Verdacht, Leiter eines Scorpion genannten Spionagenetzes in Süd- und Ostafrika zu sein.

„Usiku huo huo nikaamua kuikagua nyumba ya jasusi huyo maana nilikuwa bado sijaridhika na maelezo yake. Kwa bahati nikaipata ripoti moja iliyokuwa imefichwa chini ya zulia zito chumbani kwake. Ripoti hiyo, ilimaliza kiu yangu yote ya habari. Ilikuwa inataja majina yote ya maajenti wa Operesheni *Scorpion*. Kwa upande wa kwetu hapa, kulikuwa na majina manne, tena majina makubwa sana ... Knox James, Mwapaker, Kasongo wa *Disco Fever Haven* na Mthuni Kifuu, Kamanda Mkuu wa Polisi!“ (Uk. 136)

Kalenga hört aufmerksam zu. Hamisi ist müde, erzählt aber weiter. Er flog sofort von Nairobi nach Dar-es-Salaam. Er hat James Knox, Henry Mwapaker und Kasongo verhaften und einsperren lassen, getraute sich jedoch nicht, auch seinen Dienstvorgesetzten Kamanda Kifuu festzunehmen. Er besuchte ihn und gab an, dass er in Frankreich gewesen sei und alles gut gegangen sei. Er erfuhr, dass der Spion Botha von Kamanda Kifuu frei gelassen und die beiden Helfer von Mkela, Inspektor Maskini und Inspektor Mwaikusa, aus dem Dienst entlassen worden sind.

„Hatua hizo za Kamanda Kifuu zikanishangaza kidogo, nikaanza kupeleleza. Nikagundua kuwa alikuwa kapata habari juu ya safari yangu Nairobi kutoka kwa mtu fulani Kenya. Tena mtu huyo alimsimulia yote kuhusu jasusi Botha na McDonald pamoja na ripoti niliyokuwa nimeipata nyumbani kwa jasusi McDonald.“

„Kabla sijapumua sawasawa, nikaletwa vilevile barua ya kuachishwa kazi kutoka kwa Waziri wa Polisi, nikapigwa na butaa! Sikusema kitu, nikaongoza nyumbani kwangu, nikakuta nyumba yangu imevunjwa na kupekuliwa kila sehemu. Nikahisi kuwa walioivunja nyumba yangu walikuwa wanatafuta ripoti niliyokuwa nayo maana hakuna kitu kilichokuwa kimeibiwa,“ Hamisi akasimulia na kunyamaza kidogo.

Akaeleza kuwa majirani wake wakafika kumpa pole na kumweleza kwamba nyumba yake ilivunjwa na watu waliokuwa wamevaa nguo za Polisi.

„Nikawa na hakika kuwa Kamanda Kifuu alikuwa mbele ya yote hayo, lakini ni mateke ya mkata roho. Nikaamua kwenda moja kwa moja nyumbani kwa Waziri Chenza kumpa ripoti hiyo.“

„Kabla sijatoka nyumbani kwangu, nikasikia mlio mkali wa bunduki, nikalala chini. Mlio huo ukafuatiwa na risasi mchafu koge zilizovunja vioo vya nyumba yangu,“ Hamisi akaeleza huku Kalenga katumbua macho kwa hofu.

„Nilitambua kabisa kuwa maisha yangu yalikuwa hatarini nd'o maana nilipopata habari za kuachishwa kazi kwa vijana wangu na kuachiliwa huru kwa jasusi Botha, nikaamua kuwahamisha kina Nuru.

„Nd'o maana vilevile, nikakuambia usinipigie simu maana nilijua kuwa nimekuwa mtu wa kuwindwa kama mnyama wa porini,“ Hamisi akasema.

„Basi kwa ufupi Kalenga, nikaamua kuihama nyumba yangu. Jana nililala kwenye hoteli ya Amana lakini nikaamua kuhama usiku huo baada ya askari fulani kunimiminia risasi chumbani kwangu,“ Hamisi akasema.

„Leo niko hapa, kesho sijui nitakuwa wapi! Nimekuwa mtu wa kutangatanga tu kwa vile nataka haki itendeke. Waswahili hawa wamepania kweli kuhakikisha kuwa wanaipata ripoti hii kufa au kupona.“ (Uk. 136-137)

Hamisi gibt Kalenga einen Brief zur Überbringung an Minister Chenga. Plötzlich geht das Licht aus. Vier Gewehrschüsse sind zu hören. Hamisi und Kalenga werfen sich zu Boden. Die Schüsse treffen die Möbel und die Lampe. Es ist finster und totenstill. Kalenga ist nicht verletzt, aber Hamisi blutet. Er hört Schritte vor der Türe. Der Türschloss wird aufgebrochen. Kalenga sieht den Schatten zweier Männer mit Maschinengewehren. Das Telefon ist aber noch intakt. Kalenga ruft Minister Chenga an. Dr. Chenga macht sich sofort auf dem Weg. In zehn Minuten trifft er bereits mit drei Ärzten, sechs Polizisten und fünf Soldaten ein. Die Ärzte untersuchen die Verletzungen von Hamisi. Dr. Kiswalu beruhigt Kalenga. Hamisi ist nur leicht verletzt. Er werde schnell genesen. Hamisi wird in den Ambulanzwagen gebracht. Ein Soldat berichtet, dass die zwei Verbrecher gefasst wurden. Auch sie sind verletzt und werden in die Rettungswagen gelegt. Dr. Chenga nimmt Kalenga in seinem Auto mit.

„Mzee, samahani, hivi unaifahamu Pepo ya Mabwege?“ Kalenga akauliza.

„Unakusudia ulimbwende?“ Waziri akauliza akionyesha mshangao kidogo.

„Hapana, ulimbwende ni ulimbwende na Pepo ya Mabwege ni Pepo ya Mabwege,“ Kalenga akajibu na kumfanya Waziri aangue kicheko cha ghafla. (Uk. 139)

Minister Dr. Chenga gibt bescheiden zu, dass er den Begriff Pepo ya Mabwege nicht kenne und nicht verstehe. Er ersucht Kalenga, ihn am folgenden Tag in seinem Büro zu besuchen und ihn den Begriff zu erklären.

3. Übersetzungsübung. *Mazoezi.*

Diese kurzen Sätze sind für eine mündliche oder schriftliche Übung gedacht.

Die Braut Josina Simango und der Bräutigam Peter Knox befinden sich in einer Kirche (*kanisa fulani*) in Dar-es-Salaam.

Es ist der Tag ihrer Trauung.

Peter ist der Sohn des Ministers James Knox.

Joachim, Josinas Vater, war Gärtner (*mlimaji shamba la mboga*) des Ministers .

Die Kirche ist voll (*limejaa watu*).

Prominente Leute (*watu wa heshima*) aus Wirtschaft und Politik sind gekommen.

Pastor Maka tritt ein.

Er begrüßt die Gemeinde (*jamii/-*).

Er fragt den Bräutigam: „Peter Knox, bist du bereit, Josina Simango zu deiner Ehefrau zu nehmen?“

Der Bräutigam antwortet: „Ja!“

Er fragt die Braut: „Josina Simango, bist du bereit, James Knox zu deinem Ehemann zu nehmen?“

Die Braut antwortet: „Nein!“

Die Brille und die Bibel des Pastors fallen zu Boden (*ku-anguka chini*).

Die Kamera des Fotografen fällt zu Boden und zerschellt (*ku-pasuka vipandevipande*).

Dem Bräutigam wird es schwindlig (*ku-ona kizunguzungu*).

Die Eltern des Bräutigams sind wütend (*ku-ona ghabhabu*).

Sie gehen rasch hinaus.

Es wird still in der Kirche.

Plötzlich ertönt ein Klageschrei (*yowe/ma-*).

Josinas Mutter ist tot.

Joachim Simango lebt einsam.

Die Nachbarn nennen Josina ein Unglückskind (*kisirani/vi-*).

Joachims Bruder heisst Komba.

Er sorgt sich um (*ku-m-tunza*) Joachim.

Sie sind in Mosambik geboren.

Sie sind nach Tansania geflüchtet (*ku-kimbilia*).

Sie sind Flüchtlinge (*wa-kimbizi*).

Der ältere Bruder ist in Mosambik geblieben.

Er kämpfte gegen die Portugiesen.

Josinas Schwester heißt Nuru.

Sie geht noch zur Schule.

Sie tischt das Mittagessen für Onkel Komba auf (*ku-pakua*).

Sie bringt gute Nachricht (*habari njema*).

Gäste aus Mosambik sind angekommen.

Minister James Knox fährt (*ku-endesha*) mit einem Auto der Type Audi Fox.

Er war im Dienst.

Er fährt (*ku-elekea*) nach Hause.

Er wohnt in Oyster Bay.

Dies war zur Kolonialzeit das Europaerviertel (*uzunguni*).

Er hat eine Flugkarte (einen Flugschein) in der Aktentasche (*mfuko wa faili*).

Er läutet an (*ku-piga kengele*)

Der Hausdiener Masanja öffnet die Türe.

Seine Frau gibt ihm einen saftigen Kuss (*ku-m-piga mabusu ya motomoto*).

James Knox gibt Peter die Flugkarte (den Flugschein).

Peter wird einen ganzen Monat in den USA (*Marekani*) Urlauben (*ku-talii*).
Das Ministerium von James Knox wird den Flug, die Verpflegung (*malaji*) und die Unterkunft (*malazi*) finanzieren (*ku-gharamia*).
Ein Gast läutet an.
Er heisst „Sir“ Henry Mwapaker.
Er ist vornehm gekleidet (*ku-vaa maridadi*).
Er ist Geschäftsführer der Fabrik *Kiwanda cha Sufuria za Chai*.
Er trinkt gern Whisky und raucht *Rothmans* Zigaretten.
Er fragt: „Wer ist diese Josina?“
James Knox antwortet: „Sie ist ein Kind armer Leute“ (*mtoto wa kifukara*).
Er fügt hinzu (*kuongeza*): „Sie ist Lehrerin in der Forodhani Secondary School und 22 oder 23 Jahre alt.“
Henry Mwapaker möchte sie bestrafen.
Sie wird ihre Stelle verlieren (*ku-fukuzwa kazi*).
James Knox ist dagegen (*ku-kataa* oder *ku-pinga*).
Seine Frau ist dafür (*ku-unga mkono*).
Minister James Knox ist Sekretär des Verwaltungsausschusses der Sekundarschule Forodhani (*Katibu wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo cha Forodhani*).
Henry Mwapaker ist Leiter des Ausschusses zur Bekämpfung von Korruption (*Mkurugenzi wa Bodi ya Kupunguza Milungura*).
Mwapaker verabschiedet sich von Frau Knox und Peter.
Mwapaker und Knox gehen für ein vertrauliches Gespräch hinaus (*kongamano la siri*. Ich unterscheide zwischen *ma-zungumzo* und *ma-kongamano*).
Mwapaker kennt einen Inder namens (*anayeitwa*) Devkumar Puri.
Mwapaker soll ihn wegen Bestechung anzeigen.
Puri ist bereit, Mwapaker etwas zu bezahlen (*kulipa kitu*), wenn er die Akten (*faili/ma-*) vernichtet.
Auch Knox kennt den Inder .
Knox gibt Mwapaker den Rat, das Geld anzunehmen.
Minister James Knox sagt: „Wenn es ums Essen geht, soll man Amt und Politik beiseite lassen.“ (*Unapopatikana wasaa ya kula, mambo ya vyeo na siasa tuyaweke pembeni. Uk. 14*)
Josina geht ins Wohnzimmer.
Ihr Onkel aus Mosambik umarmt und küsst sie.
Er nennt sie Lulu (Perle).
Ihre Eltern haben ihr diesen Namen gegeben.
Jetzt nennt sie sich Josina.
Josina war Freiheitskämpferin (*mpigania uhuru*) in Mosambik.
Kalenga ist das neunte Kind von Sheikh Mabruki.
Er ist das Letzgeborene (*kitinda mimba*, ein Kind, das den Mutterschoss schliesst.)
Sein Vater hatte vier Frauen.
Sie brachten acht Mädchen zur Welt.
Sheikh Mabruki war traurig (*ku-ona uchungu*).
Endlich (*hatimaye*) gebar eine Frau einen Sohn.
Sheikh Mabrukis Freude war grenzenlos (*furaha isiyo na kifani*).
Josina fährt mit dem Bus zur Arbeit (*kazini*).
Ein junger Mann spricht sie mit dem Namen Lulu an (*ku-zungumzia*).
Sie erkennt ihn.
Sie nennt ihn Akida.

Die *Akidas* waren Arbeitsaufseher (*m-nyampara*) der Deutschen.
Die *Akidas* waren zumeist Araber (*wengi wao walikuwa*).
Sheikh nannte seinen Sohn Akida.
In Forodhani legte Akida diesen Namen ab (*ku-acha*).
Er nennt sich jetzt Kalenga.
Kalenga war die Festung (*ngome*) des Königs Mkwawa.
Er hat gegen die Deutschen gekämpft.
Josina und Kalenga gingen (*ku-soma*) auf die *St. Joseph's Secondary School*.
Jetzt heisst die Schule *Forodhani*.
Joakim und Binamu diskutieren über das neue Mosambik.
Frauen stehen dort im Vordergrund (*mstari wa mbele*).
Binamu nimmt Josina in Schutz.
Sie hatte das Recht, ihren Ehemann selber auszusuchen.
Joachim ist dagegen (*ku-kataa* oder *kupinga*).
Josina und Kalenga warten auf den Bus.
Ein Mercedes-Benz hält vor ihnen.
Ein alter Herr mit Glatze und einem Wohlstandsbauch (*kitambi cha starehe*) lädt (*ku-m-karibisha*) Josina zum Einsteigen ein.
Sie lehnt zornig ab.
Ein junger Mann und ein junges Mädchen warten auf den Bus.
Ein Toyota Corolla hält vor ihnen.
Der Herr bittet das Mädchen einzusteigen.
Sie fährt mit (*ku-safiri naye*).
Josina und Kalenga sitzen im *Hilton Beach Hotel*.
Ein Kellner (*m-hudhumi*) heisst sie willkommen.
Sie bestellen *Samusas, Kebab* und Getränke.
Der Kellner verlangt Vorauszahlung (*malipo ya kutangulia*).
Die Touristen (*watalii*) zahlen erst nach dem Essen.
Josina und Kalenga haben jetzt Zeit (*wana nafasi*), in Ruhe (*kwa raha*) miteinander zu reden.
Nach Beendigung (*ku-timiza*) des *Form IV* studierte Josina Sozialwissenschaften (*Taaluma ya Jamii*) in Kuba.
Danach bekam sie (*ku-ajiriwa* oder *ku-pata kazi ya*) einen Lehrerinnenposten an der *Forodhani Secondary School*.
Peter hat auch diese Schule besucht.
Er liebt Josina.
Sie liebt ihn nicht.
Eines Tages (*siku moja*) sagte er ihr: „Komm zu mir (*karibu kwangu*).“
Er fügte hinzu (*ku-ongeza*): „Wir werden die Vorbereitungen (*ma-andalio*) für unsere Hochzeit besprechen.“
Sie erfuhr (*ku-pata habari*) später, dass sogar der Tag schon festgelegt war.
Joachim Simango freute sich, dass seine Tochter den Sohn eines Ministers heiratet.
Josina suchte Minister James Knox in seinem Büro auf.
Er riet ihr (*ku-pendekeza, ku-m-pendekez-e-a*) diese günstige Gelegenheit (*nafasi/-, uteuzi*) wahrzunehmen (*ku-shiriki*).
Die Ehe mit Peter wird ihr helfen, weiterzukommen (*ku-ji-endeleza*).
Kalenga hat nicht viel zu erzählen.
Im Jahre 1975 wurde Mosambik frei.
Er arbeitete dort als Journalist (*mwandishi wa habari*).

Jetzt ist er Redakteur (*m-hariri/wa-*) der Tageszeitung *Kioo cha Bia*.
Josina ist in ihrem Elternhaus zurück.
Sie ist arbeitslos (*hana kazi*).
Sie hat die Stelle in *Forodhani* verloren (*ku-fukuzwa kazi*).
Kalenga kommt zu Besuch.
Er liest die Kündigung (*hati/-* oder *barua/- ya kufukuzwa kazi*).
Kalenga geht zurück zur Arbeit.
Der Chefredakteur erwartet ihn.
Er sagt: „Josina ist entlassen worden.“
Er gibt ihm den Bescheid.
Er möchte ihn in *Kioo cha Bia* veröffentlichen (*ku-tolea*).
Kalenga lehnt seinen Vorschlag ab.
Kalenga fährt mit dem Dienstwagen nach Hause.
Er wird von einem Polizisten aufgehalten (*ku-simamishwa*).
Er wird wegen Fahrens in alkoholisiertem Zustand verurteilt.
Er bleibt zwei Tage in Haft.
Der Entlassungsbescheid erschien in *Kioo cha Bia*, als er im Gefängnis war.
Josina und Kalenga sitzen im Hotel Amana.
Ein Gast kommt herein.
Alle Angestellten nehmen Haltung an, stehen Habtacht (*ku-simama wima*).
Es ist Peter Knox.
Peter, Josina und Kalenga Sie plaudern gemütlich.
Sie hatten einander in *Forodhani* kennen gelernt (*ku-fahamiana*).
Ein Europäer tritt ein.
Peter steht auf und eilt zu ihm (*ku-m-kimbilia*).
Kalenga arbeitet in seinem Büro.
Chefredakteur Bubu Ogola kommt herein.
Er teilt ihm mit (*ku-m-pasha habari* oder *ku-m-w-arifu*), dass Minister James Knox ihn sehen will.
Kalenga befindet sich im Büro des Ministers James Knox.
Minister James Knox verabschiedet sich von den drei Männern, die bei ihm waren.
Sie alle tragen graue Anzüge.
Minister Knox heisst Kalenga in seinem Büro willkommen.
Die Besprechung ist kurz.
Er ist auch Vorsitzender des Rates für Disziplin am Arbeitsplatz (*Konseli ya Nidhamu ya Wafanayakazi Nchini*).
Viele Beschwerden (*ma-lalamiko*) gegen Kalenga sind bei ihm eingelangt.
Er fordert (*ku-amuru*) Kalenga auf, sein Verhalten (*m-w-enendo/mi-*) zu ändern.
Kalenga möchte mit seinem Dienstauto nach Hause fahren.
Es steht nicht da.
Kalenga sieht einen Jungen, der Erdnüsse verkauft.
Dieser heisst Kitwana.
Er ist ein Waisenkind.
Er war dort, als Kalenga mit (*katika*) seinem Auto ankam.
Er sah drei Männer mit dem Auto wegfahren.
Sie trugen graue Anzüge.
Kalenga bringt (*ku-fikisha*) Kitwana in seine Wohnung.
Er sorgt für ihn.

Kalenga meldet (*ku-toa ripoti*) bei der Polizei, dass sein Auto gestohlen wurde.
Der Polizist fragt: „Hast du jemanden in Verdacht?“
Kalenga antwortet: „Minister James Knox.“
Der Polizist ruft den Postenkommandanten (*Kamanda ya Kituo*).
Dieser glaubt Kalenga nicht.
Der Polizeidirektorstellvertreter kommt herein.
Er heisst Hamisi Mkela
Alle drei Polizisten stehen stramm und salutieren (*ku-piga saluti*).
Er liest Kalengas Bericht.
Er befiehlt dem Postenkommandanten, den Fall (*kesi*) sofort bei Gericht anhängig zu machen (*ku-fikisha mahakamani*).
Er erkennt Kalenga.
Sie waren Freunde in *Forodhani*.
Minister James Knox erscheint am nächsten Tag (*siku ifuatayo*) vor Gericht.
Am gleichen Tag verliert Joachim Simango die Bewilligung, sein Geschäft zu führen.
Josina sitzt am Strand.
Peter kommt vorbei.
Er liebt Josina wirklich (*kwa dhati*).
Er sagt ihr: „*Pendo ni kama mkondo. Ni vigumu zulizuia.*“
Er ist der Sohn eines Ministers.
Sie ist die Tochter des Gärtners des Ministers.
Sie antwortet: „*Mpanda ngazi na mshuka ngazi, kamwe hawashikani mkono.*“
Sie passen nicht zusammen (*ku-lingana*).
Er fragt: „Liebst du Kalenga?“
Sie antwortet nicht.
Kalenga besucht Hamisi Mkela in seiner Wohnung in Changombe.
Hamisi wurde in Moskau zum Militärpiloten ausgebildet.
Kalenga berichtet von Devkumar Puri.
Puri hatte einem Beamten der *Benki ya Uchumi* bestochen (*ku-m-pa rushwa*).
Puri wollte Waren aus dem Ausland einführen.
Der Beamte sollte sein Ansuchen beschleunigt erledigen (*ku-pitisha kwa haraka*).
Beide wurden von der Polizei verhaftet.
Beide wurden eingesperrt.
Nach einer Woche wurden beide freigelassen.
Der Fall wird der Korruptionsbekämpfungsbehörde (*Bodi ya Kupunzuga Milungura*) übergeben.
Der Vorsitzende des Ausschusses ist Henry Mwapaker.
Mwapaker besucht Puri bei Nacht (*saa za usiku*).
Er droht Puri mit einer Haftstrafe.
In der folgenden Nacht kommt er wieder.
Er verspricht die Akten zu vernichten, falls Puri ihm einen gewissen Betrag (*kiasi fulani cha Fedha*) gibt.
Er soll das Geld sofort Minister James Knox überbringen (*a-m-pe*).
Puri stimmt zu.
Hamisi fragt: „Wie hat er das Haus von Knox erkannt?“
Kalenga antwortet: „Es geschah nicht zum ersten Mal.“
Hamisi gibt zwei Polizisten den Auftrag, Knox und Mwapaker zu beobachten.
Kalenga ist wieder in seiner Wohnung.
Kalenga ruft Hamisi um 21 Uhr an.

Kalenga berichtet, dass er entlassen worden ist, weil ihm das Dienstauto abgekommen ist.
Man behauptet (*wanadai*) auch, dass er betrunken gefahren sei.
Kalenga bittet um seinen Rat.
Hamisi gibt ihm den Rat, die Entlassung anzunehmen und zu schweigen.
Onkel Binamu und seine Frau fliegen (*ku-safiri kwa ndege*) nach Mozambik.
Josina besucht Kalenga.
Sie hofft Hamisi Mkela dort kennenzulernen (*ku-fahamiana na*).
Sie hofft, dass er ihr Arbeit geben kann.
Die Parlamentswahlen stehen bevor (*zi-na-karibia*).
James Knox kandidiert (*ku-gombea kiti*).
Hamisi wurde befohlen, dienstlich nach Frankreich zu reisen.
Kalenga hat einen Geheimplan.
Der Chefredakteur Bubu Ogola ist auf Reisen.
Kalenga möchte einen Bericht über Korruption in der Oberschicht veröffentlichen.
Auch James Knox und Henry Mwapaker gehören zu ihnen.
Er geht ins Büro und bereitet alles vor (*ku-andaa*).
Er kommt in seine Wohnung zurück.
Josina erwartet (*ku-subiri*) ihn.
Zum ersten Mal sprechen sie über Liebe und Ehe.
Die Morgenausgabe (*toleo /ma*) von *Kioo cha Bia* erscheint.
Alle Exemplare sind schnell ausverkauft.
James Knox sitzt in seiner Wohnung.
Er schwitzt.
Er ist außer sich (*ana kichaa*).
Seine Frau macht sich in der Wohnung zu schaffen (*ku-randaranda*).
Der Hausdiener Masanja kommt nicht zur Arbeit.
Knox und seine Frau machen sich auch Sorgen über Peter.
Die ganze Nacht (*usiku kucha*) ist er mit dem *Audi Fox* unterwegs.
Der Chauffeur kommt.
Er möchte Minister James Knox zu seiner Wahlveranstaltung (Wahlen *uchaguzi*) bringen.
James Knox kommt aber nicht mit.
Mwapaker lebt in Angst.
Bei James Knox läutet es.
Von drei Polizisten begleitet, tritt Hamisi Mkela ein.
James Knox wird zur Polizeistation (*kituo cha Polisi*) gebracht.
Seine Frau fällt in Ohnmacht (*ku-zirai*).
Kalenga sitzt in der Wohnung seines Vaters.
Er liest die Zeitung.
Er denkt an die Nacht im Hotel Amana, in der Hamisi und er den Spion Piet Botha beobachteten.
Botha spionierte für Südafrika.
Tansania unterstützte den Freiheitskampf in Südafrika.
In dieser Nacht tauschten Botha und Knox Aktentaschen aus.
Hamisi und Kalenga verfolgten (*ku-m-fuata*) Botha bis ins Kilimanjaro Hotel.
Dort wurde Botha verhaftet.
Kalengas Vater wurde die Bewilligung entzogen, ein Geschäft zu führen.
Er und seine Frau haben kein Einkommen.
Vier Polizisten in Begleitung von Chefredakteur Bubu Ogola verhafteten Kalenga.
Sie fahren zum Ministerium für Politik und Staatssicherheit.

Der Minister heisst Dr. Chenga Karl Chenga.
Er erkennt Kalenga.
Er hat Mosambik dienstlich (*ki-kazi*) besucht, als Kalenga dort als Reporter (Journalist) arbeitete.
Kalenga werden die Handschellen abgenommen.
Dr. Chenga gratuliert ihm.
Es ist ihm gelungen, Korruption aufzudecken und den Spion Botha zu fassen.
Er wird zum Chefredakteur von *Kioo cha Bia* ernannt.
Kalenga möchte seinen Eltern diese Nachricht überbringen.
Er möchte aber zuerst mit Josina sprechen.
Sie bleiben ein wenig abseits von Josinas Haus stehen.
Zwei Polizeiwagen, ein Rettungswagen und ein *Audi-Fox* stehen vor dem Haus.
Kalenga steigt aus (*ku-telemka*).
Kalenga läuft schnell zur Wohnung Josinas (*ku-i-kimbilia nyumba ya Josina kwa kasi*).
Inspektor Maskini begleitet ihn.
Kalenga sieht drei Leichen, die mit weissen Tüchern (*shuka/ma-*) zugedeckt sind.
Kalenga fragt Hamisi Mkela: „Wo ist Josina?“
Mkela antwortet: „Josina, Joachim Simango und Peter Knox sind tot.“
Peter Knox drang in das Schlafzimmer von Josina ein.
Er hat sie erschossen.
Danach erschoss er sich selbst.
Als der Vater von Josina ihre Leiche sah, starb er auch.
Alle drei Leichen werden ins Spital gebracht.
Nuru wird in Hamisi Mkelas Privatwohnung gebracht.
Hamisi fährt mit dem Polizeiwagen weg.
Kalenga bleibt mit den Nachbarn zurück.
James Knox und Henry Mwapaker sind in Haft.
Ihr Fall wird untersucht (*ku-peleleza*).
Die Anklage lautet auf Landesverrat, Veruntreuung von Volkseigentum (*mali ya umma*) und Korruption.
Kalenga wohnt seit drei Tagen in der Wohnung des Chefredakteurs.
Nuru und Kitwana wohnen bei ihm.
Sie schlafen.
Es ist Nacht.
Hamisi Mkela ruft an (*ku-piga simu*).
Er bittet Kalenga, sofort ins Hotel Misakato zu kommen.
Sie verstecken sich in einem kleinen Zimmer beim WC.
Mkela hat viel zu berichten.
Er erhielt den Auftrag nach Frankreich zu reisen.
Es gab einen Geheimplan, ihn dort zu töten.
Er blieb in Nairobi.
Er berichtete (*ku-arifu*) der Polizei in Nairobi, dass der Spion Botha in Dar-es-Salaam festgenommen wurde.
Mkela suchte nach einem gewissen (*fulani*) McDonald in Nairobi.
Er leitete das Spionageprogramm (*ratiba ya ujasusi*) für Süd- und Ostafrika.
Das Programm heisst *Scorpion*.
Die Polizei durchsucht seine Wohnung.
Unter dem Teppich fanden sie ein Heft mit den Namen der Mitarbeiter.
In diesem Heft waren folgende (*yafuatayo*) Namen zu finden: (*yaani* = nämlich) James Knox,

Henry Mwapaker, Kasongo von *Disco Fever Haven* und Polizeidirektor Mthuni Kifuu.
Mkela kehrte nach Dar-es-Salaam zurück.
Er erfuhr, dass der Spion Botha freigelassen wurde.
Die zwei Mitarbeiter Mkelas, nämlich Maskini und Mwaikusa wurden entlassen.
Auch Hamisi Mkela wurde entlassen.
Seine Wohnung wurde von der Polizei durchsucht.
Das Heft mit den Namen der Mitarbeiter von *Scorpion* fanden sie nicht.
Hamisi hat jetzt keinen festen Wohnsitz.
Er fürchtet (*ku-hofia*) um sein Leben.
Mkela übergibt Kalenga einen Brief an Dr. Chenga.
Plötzlich geht das Licht aus.
Gewehrschüsse (*mlio wa bunduki*) sind zu hören.
Kalenga ist unverletzt.
Mkela blutet (*ku-toa damu*).
Kalenga ruft Dr. Chenga an.
In kurzer Zeit ist er da.
Er wird von drei Ärzten, sechs Polizisten und fünf Soldaten begleitet.
Hamisi wird ins Spital gebracht.
Die zwei Männer, die Hamisi angeschossen (*ku-piga risasi*) hatten, sind gefasst.
Dr. Chenga nimmt Kalenga in seinem Auto mit.
Kalenga fragt ihn: „Verstehen Sie die Bedeutung von 'Pepo ya Mabwege' ?“
Dr. Chenga Karl Chenga antwortet: „Nein!“.

